Siasa

**THRDC: Haki, suluhu kesi ya Lissu viharakishwe**

Uk. 16

Tahariri

**Tanesco iwezeshwe kukamilisha furaha ya JNHPP**

Uk. 2

Mzee Tai

**Gavana Chalamila, abiria siyo makontena**

Safu Uk. 5


# Pambazuko

Toleo Namba 179 Jumatatu, Agosti 24-30, 2026


# Yaliyojificha nyuma ya simu za mkopo

Uk. 6&7

- BoT yatoa onyo wasio na leseni

# Mawakili kupambana kumnasua Rais Samia Kesi ya Lissu



“Kwa hiyo hakuna haja ya kuwaita mashahidi hao ambao kwa kuwa ushahidi wao umeshatolewa na watumishi wa serikali, ni kama vile anataka hawa wafike ili afanye cross examination (awafanyie mahojiano) ya kile kilichoelezwa na mashahidi hao,” alisema.

Uk. 12

## Muafaka Z’Bar waendelea kukamilishwa

Habari Uk. 21

Tafakuri ya Bagonza

## Haya yalikuwa makosa ya kimkakati, yamepokonya fursa!

Safu Uk. 10

## Wasira ahimiza vikao CCM, kujitambua

Habari Uk. 20

## Serikali yachunguza CT-Scan Aga Khan

Uk. 15

## Tahariri

# Tanesco iwezeshwe kukamilisha furaha ya JNHPP

UZINDUZI rasmi wa Bwawa na Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Julius Nyerere (JNHPP), uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan Agosti 22, 2026, ni hatua ya kihistoria inayostahili pongezi kutoka kwa kila anayeitakia mema Tanzania.

Kimsingi, huu siyo ushindi wa serikali pekee, bali mafanikio ya taifa lililothubutu kutumia rasilimali zake kujenga msingi wa uchumi wa kisasa.

Kwa uwezo wa kuzalisha megawati 2,115 kupitia mitambo tisa, kila mmoja ukiwa na uwezo wa megawati 235, JNHPP ni mradi mkubwa kuliko yote ya uzalishaji umeme nchini na miongoni mwa miradi mikubwa ya kuzalisha umeme Afrika.

Umegharimu takribani Shilingi trilioni 7.452, fedha zilizotolewa na Serikali ya Tanzania, na umeongeza uwezo wa mitambo ya taifa kuzalisha umeme kufikia karibu megawati 4,075. Zaidi ya nusu ya uwezo huo sasa inatokana na JNHPP pekee.

Hata kabla ya kuzinduliwa rasmi na Rais Samia, matokeo yake tayari yanaonekana. Katika kipindi hadi Mei 31, 2026, kituo hiki kilichangia asilimia 44.9 ya umeme wote uliozalishwa na kuingizwa katika Gridi ya Taifa.

Hiyo ni hatua kubwa katika kuondoa historia ya mgao, kuipa sekta ya viwanda uhakika wa uzalishaji, kuvutia uwekezaji na kuwezesha huduma za afya, elimu, maji, mawasiliano pamoja na biashara ndogo zinazotegemewa na mamilioni ya Watanzania.

Sisi Pambazuko tunahimiza kuwa shangwe za uzinduzi zisifanye tusahau ukweli mmoja; kuzalisha umeme mwingi ni nusu tu ya kazi. Umeme hauna faida ukiishia kwenye mitambo ya Rufiji, unapotea njiani au hauwafikii wananchi na wawekezaji kwa ubora unaotakiwa.

Sasa ni wakati wa kuhamisha nguvu ya kitaifa kutoka kwenye uzalishaji kwenda kwenye usafirishaji na usambazaji.

Takwimu za Mamlaka ya Udhibii wa Nishati (Ewura) zinaonyesha kuwa hadi Juni 2025, Tanzania ilikuwa na kilomita 8,303.87 za njia za kusafirisha umeme na vituo 72 vya Gridi ya Taifa.

Mtandao wa usambazaji unaomilikiwa na Tanesco ulikuwa na zaidi ya kilomita 213,278, lakini katika mwaka wa fedha 2024/25, shirika hilo la kusambaza umeme lilipoteza asilimia 13.86 ya nishati katika mifumo ya usafirishaji na usambazaji.

Hata kama baadhi ya viwango hivyo vilikuwa ndani ya malengo ya udhibiti, kupoteza sehemu hiyo ya umeme unaozalishwa kwa gharama kubwa siyo jambo la kupuuzwa.

Tunaitaka serikali kuiwezesha Tanesco kifedha na kitaalamu kubadilisha transfoma zilizochakaa, kuongeza njia za msongo mkubwa, kujenga vituo vipya, kuweka mifumo janja ya kupima na kufuatilia umeme, na kufanya matengenezo kabla ya hitilafu.

Uwekezaji huo uende sambamba na uwazi katika ununuzi, usimamizi wa kitaalamu, uwajibikaji wa watendaji na huduma bora kwa wateja.

Pia, umeme huu utumike kuchochea viwanda, kilimo cha umwagiliaji, uchakataji wa mazao, uchimbaji madini na uchumi wa kidijitali.

Wananchi wa vijijini na pembezoni wasiishie kusikia idadi ya megawati; waone umeme wa uhakika majumbani, shuleni, vituo vya afya na kwenye shughuli za uzalishaji.

Aidha, Tanesco ipewe uwezo wa kusawazisha uzalishaji na mahitaji, kujenga hifadhi za nishati na kuunganisha vyanzo vingine vya gesi, jua na upepo.

Pambazuko tunaamini kuwa JNHPP ni nguzo kuu, lakini usalama wa nishati unahitaji mfumo unaohimili ukame, mafuriko na hitilafu kubwa.

JNHPP ni fahari ya Tanzania, lakini kipimo chake cha mwisho hakitakuwa ukubwa wa bwawa wala gharama ya ujenzi, bali kitakuwa viwanda vinavyofunguliwa, ajira zinazozaliwa, biashara zinazokua, Ankara ambazo wananchi wanazimudu na kukoma kwa kukatika umeme.

Baada ya uzinduzi, kazi kubwa sasa ni kuhakikisha kila megawati inafika inapohitajika na kubadilisha maisha ya Watanzania na wawekezaji.

# Stendi ya Magufuli...




*Abiria wa basi la ABC wakisubiri kupakia mizigo katika Stendi Kuu ya Mabasi ya Magufuli baada ya mabasi yote kulazimishwa kuhamia hapo kutoka kwenye vituo vyao vilivyopo Shekilango, Manzese na maeneo mengine, jijini Dar es Salaam jana. (Picha na Pambazuko).*


## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**



## TIMU YA PAMBAZUKO

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Mhariri Mkuu** | : | Simon **MKINA** | (simon@pambazuko.or.tz) |
| **Mhariri Mtendaji** | : | Peter **NYANJE** | 0784 211 716 |
| **Mwandishi Mkuu** | : | Elizabeth **HOMBO** | 0712 792 216 |
| **Mwandishi Mwandamizi** | : | Andrew **MSECHU** | 0769 415 815 |
| **Mkuu wa DTP** | : | Yassin **LUPATU** | 0782 009 971 |
| **Mkuu wa Utawala** | : | Tryruckia **MFINANGA** | 0744 768 263 |

*Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz*

# Dunia: Hapa na Pale

## Dhamira pete ya uchumba

MICHERRE Fox (31) amedhihirisha msemo huu; "penye nia, pana njia," baada ya kunuia kupata pete ya kushika uchumba, bila kununua kwa sonara.

Mmarekani huyo alinuia kupata pete ya almasi kwa kuisaka mwenyewe ardhini na siyo kununua dukani ili kumvisha mchumba wake Trevor Ballou.

Alijitosha kwenye machimbo ya Murfreesboro, eneo la Arkansas, na kuanza kusaka ndoto yake, na ndani ya wiki tatu, akaibua almasi yenye uzito wa karati 2.3.

Furaha yake haikuwa kifani na alishukuru nafsi yake kwa kupigania ndoto yake na hatimaye kufanikisha matamanio yake.

## Sayansi ya vita balaa

USALAMA wa binadamu unaendelea kuwa shakani baada ya wataalamu wa vita kuendelea kujipanga kutengeneza silaha kali zaidi.

Mabadiliko zaidi yanaendelea ya kutengeneza silaha za nyuklia, vilipuzi, silaha nzito, makombora ya masafa marefu, na ndege za kasi kwa kutumia teknolojia ya silaha zisizoonekana, kupitia akili unde, umeme, na anga ya juu hivyo kupunguza nguvu ya matumizi ya risasi. Wataalamu wameelekeza nguvu zao katika silaha za miale, mawimbi ya umeme, akili unde, silaha za sauti, bunduki za kielektroniki zinazotumia makombora ya chuma, miale ya joto, mashambulizi yanayotumia satelaiti, ndege zisizo na rubani na silaha za akili na neva.





## Rais Biya arejea Ikulu

RAIS wa Cameroon, Paul Biya (93) amerejea nchini humo baada ya kukaa nje ya nchi kwa zaidi ya miezi miwili, hali iliyozua maswali kuhusu afya yake na mustakabali wa ombwe la uongozi.

Biya aliwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Yaoundé kutoka Geneva, Uswisi mwishoni mwa wiki, baada ya kukaa nje ya nchi kwa zaidi ya wiki 10.

Kiongozi huyo, anayetajwa kuwa rais mwenye umri mkubwa zaidi duniani, aliondoka Cameroon Juni 7 kwa kile ofisi yake ilichokiita "mapumziko mafupi ya binafsi barani Ulaya."

## Hofu vurugu za uchaguzi

WANANCHI wa Kenya wameanza kuonyesha hofu yao kuwa huenda kukaibuka vurugu za uchaguzi wakati wa Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Agosti, 2027.

Hofu hiyo inazidi kuongezeka kutokana na vurugu zilizoibuka kwenye maeneo ya Homa Bay kabla ya mkutano wa upinzani wiki iliyopita, ambapo baadhi ya watu waliokuwa wamebeba marungu na mapanga walifunga barabara, kuchoma matairi, kushambulia wapita njia na kupora mali.

Tayari Wakfu wa Kofi Annan unaonya kuwa Kenya ina uwezekano mkubwa wa kushuhudia vurugu za uchaguzi mwaka 2027, ikikadiriwa kuwa Kenya ina uwezekano wa asilimia 84.1 wa kushuhudia aina fulani ya vurugu za uchaguzi japokuwa siyo lazima zitokee.

Na Mzee TAI

# Gavana Chalamila, abiria siyo makontena

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, ameamua kwamba mabasi yote yaendayo mikoani yaanzie na kuishia Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli, Mbezi Luis.

Kwa tafsiri rahisi, basi lisimfuate abiria Sinza, Shekilango, Mabibo au sehemu nyingine iliyo karibu naye. Abiria ndiye afuate basi, hata kama safari ya kulifuata inahitaji safari nyingine yenye foleni, mizigo na gharama ya ziada.

Hapo ndipo Dar es Salaam inapogeuzwa darasa la mazoezi ya uvumilivu. Mama mwenye watoto wawili na mabegi matatu kutoka Mbeya ashushwe Mbezi, halafu aambiwe aende Kigamboni kwa daladala, mwendokasi au bajaji.

Mzee anayekwenda hospitali Tabata naye aanze kwanza ziara ya kutalii jiji. Inaonekana tiketi ya basi sasa itakuja na somo la lazima la kubeba mizigo kwa kichwa.

Chalamila anasema wanaopanda ndege huifuata uwanja wa ndege na wanaotumia SGR huenda stesheni; kwa hiyo na wa mabasi waende Kituo cha Magufuli.

Mfano huo unasikika vizuri jukwaani, lakini umejaa maswali mengi. Chalamila anatambua kabisa kuwa ndege haiwezi kutua Shekilango, wala treni kugeuza reli na kumfuata abiria Manzese.

Basi, tofauti na ndege na treni, linatumia barabara zilizopo na linaweza kupakia kwenye kituo kilichoidhinishwa bila kuvuruga safari.

Aidha, viwanja vya ndege na vituo vya reli hujengwa pamoja na mipango ya usafiri unganishi. Kama Magufuli inataka kuwa "uwanja wa ndege wa mabasi," basi ipewe kwanza teksi za bei nafuu, mwendokasi wa kutosha, nafasi ya mizigo, maegesho, usalama, vyoo na njia za haraka kwenda maeneo yote ya jiji.

Mimi kwa kuwa nimekuwa mtumishi wa serikali na sasa nimestaafu, nafahamu mantiki ya kuondoa vituo bubu, kudhibiti foleni, kukagua mabasi na kuhakikisha mapato ya serikali hayapotei.

Lakini Gavana Chalamila na wakubwa wenzake wa jiji wanapaswa kutambua kuwa dawa ya kupooza maumivu ya kichwa siyo kukata kichwa.

Taarifa za waendeshaji zinaonyesha kituo kina takribani nafasi 108 za maegesho, wakati mabasi yanaweza kuzidi 400 kwa siku na kufikia 800 msimu wa sikukuu.

Kuyakusanya yote hapo kunaweza kuhamisha msongamano kutoka katikati ya jiji na kuupeleka Mbezi, kisha tukatangaza tumeshinda foleni kwa kuihamisha tu anwani.

Tatizo jingine ni gharama iliyofichwa, inawezekana abiria akiongezewa nauli ya kufika Mbezi au kutoka huko, muda wa safari na malipo ya kubeba mizigo, bei hiyo haiandikwi kwenye tiketi, lakini inatoka mfukoni mwake.

Mfanyabiashara mdogo anayesafirisha bidhaa naye ataongeza gharama hiyo kwenye bei ya bidhaa. Mwishowe, agizo linalodaiwa kuleta nidhamu linaweza kuwa kodi isiyoandikwa kwa maskini.

Serikali haipaswi kumrahisishia msimamizi kazi kwa kumtwisha mwananchi mzigo. Huo siyo utawala bora.

Sasa suluhisho siyo kuruhusu kila basi kusimama popote. Jiji liidhinishe vituo vichache vya kampuni vinavyokidhi masharti ya eneo, usalama, vyoo na maegesho.

Mabasi yaruhusiwe kushusha au kupakia kwa muda maalumu bila kuegesha barabarani, huku ukaguzi mkuu ukifanyika Stendi ya Magufuli. Ratiba, tiketi na vituo visimamiwe kidijitali ili wanaokiuka waadhibiwe. Uongozi mzuri haupimi mafanikio kwa kuona kituo kimejaa mabasi; hupima kama wananchi wamepunguziwa muda, gharama na mateso.

Chalamila aelewe kuwa abiria siyo makontena ya kukusanywa bandarini. Ni watu wenye watoto, mizigo, uzee, ulemavu, miadi na fedha kidogo.

Kwa hiyo, Chalamila – katika jambo hili, amepotoka siyo kwa kutaka utaratibu, bali kwa kudhani utaratibu lazima uume.

Gavana Chalamila anapaswa kuisikiliza Dar na watu wake kabla Dar haijamjibu kwa honi, foleni na mabegi yanayoburuzwa.

Huduma ya usafiri imejengwa kumfuata mwananchi kwa mipango, siyo kumshikisha adabu – kama kweli anastahili, kwa kumchosha.

■ Habari Kuu

# Yaliyojificha nyuma ya simu za mkopo




Na Elizabeth HOMBO

HIVI sasa ukipita katika maeneo mengi yenye misongamano mijini, lazima ukutane na kelele za matangazo ya simu za mkopo.

Mbali na kuwa na maduka, wakopeshaji wa simu za mkononi wengine wameegesha vibanda wakitangaza kuwa na huduma hiyo kama wanavyofanya baadhi kwa kuchomeka miamvuli kwenye meza na kugeuza kituo cha kukopesha simu.

Hawa wote huwavuta zaidi watu wenye kipato cha chini, kuchangamkia 'fursa' hii, wakiamini katika masharti ambayo kwa "haraka-haraka" yanaonekana kuwa nafuu sana, lakini ukizama kwa ndani yana maumivu makubwa kwa wakopaji.

Kuna mengi yaliyojificha katika 'biashara' hii inayozidi kukua kila siku katika miji mikubwa hasa Dar es Salaam.

Mathalan, wakati wakopeshaji hawa wakionyesha kuwa gharama za kupata simu ni ndogo – wao wanaiita kianzio, lakini ukikokotoa hesabu ya fedha zote mteja anazolipa hadi anakamilisha kulipa deni lake la simu, unabaini kuwa simu hiyo inakopeshwa hadi mara mbili hadi tatu ya thamani yake halisi iwapo itanunuliwa kwa fedha taslimu.

**Masharti magumu zaidi**

Gharama hiyo imejificha katika riba ya mkopo huo ambao hulipwa kupitia makato ya kila siku au wiki na masharti magumu ya umiliki wa kifaa hicho kabla ya mteja hajamaliza deni.

Kati ya masharti ambayo mkopaji anatakiwa kuyakamilisha ili kustahili kukopeshwa simu ni kuwa na kitambulisho cha taifa, mdhamini mmoja na kianzio kutegemea na aina ya simu. Lakini akishakopeshwa simu, anatakiwa kuanza kulipa deni hilo ndani ya wiki moja!

**Matakwa ya sheria**

Haya yanatokea wakati serikali imeshatunga sheria mahususi kusimamia masuala ya mikopo.

Hii ni Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha (Microfinance Act, 2018) ambayo ndiyo sheria kuu inayosimamia taasisi zote zinazotoa mikopo midogo. Hawa wanaotoa mikopo ya simu wanaangukia katika uratibu na usimamizi wa sheria hii.

Sheria hiyo inataka kila mtoa mkopo kuwa na leseni halali kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inayomruhusu kufanya shughuli hiyo na kwamba kutoa mkopo bila kibali ni kosa la kisheria.

Pia Kanuni za Ulinzi wa Mtumiaji wa Huduma za Fedha (BoT Financial Consumer Protection Regulations), zinalinda wakopaji dhidi ya riba na tozo zisizoeleweka, udanganyifu au masharti ya siri.

Vilevile zinataka wakopeshaji waeleze wazi riba, ada zote na masharti ya mkopo kwa mtu anayehitaji mkopo.

Hata hivyo, pamoja na matakwa hayo ya sheria, uchunguzi uliofanywa na Pambazuko kwa miezi kadhaa sasa umebaini kuwa wakopeshaji wengi hawafuati masharti haya ya kisheria na kikanuni.

Uchunguzi umebaini kuwa wengi wa wakopeshaji simu hujipangia riba zao wenyewe na masharti yao ambayo baadhi yake hayaendani na matakwa ya sheria na kanuni.

Ufuatiliaji uliofanywa na Pambazuko kwa kujifanya ni mteja anayetaka kukopeshwa simu, umebaini kuwa wakopeshaji wengi hawako wazi kwa

Inaendelea Uk. 7

# Yaliyojificha nyuma

Inatoka Uk. 6

wateja kuhusu riba, tozo na adhabu za kukiuka masharti ya mikopo yao, jambo linalowaumiza wananchi wengi wanaokopa simu hizo.

**Maumivi kwa wakopaji**

Uchunguzi uliofanywa na Pambazuko, umebaini kuwa kwa mfano simu yenye thamani ya Shilingi 450,000 kwa fedha taslimu inaweza kumgharimu mteja zaidi ya Shilingi 800,000 baada ya kumaliza makato ya kila siku au wiki kwa mwaka mzima.

Chini ya utaratibu waliojiwekea wengi wa wakopeshaji simu hao, mteja hulazimika kulipa kwa mujibu wa makubaliano na muuzaji na pale anapokiuka masharti anafungiwa simu hadi atakapofanya malipo.

Kwamba simu haitakuwa mali ya mteja hadi malipo ya mwisho yatakapokamilika na wakati wote mkopeshaji anakuwa ndiye mdhibiti wa simu husika kiteknolojia.

Mara nyingi, mtu akishindwa kulipa ndani ya muda simu yake hufungiwa na mkopeshaji.

Hali hiyo ya mkopeshaji kuwa na udhibiti wa simu kunatia hofu baadhi ya wakopaji wakihisi kuwa mkopeshaji huyo anaweza pia kuingilia au kuangalia taarifa na data zao nyingine kwenye simu.

Wananchi wengi wamekuwa na hofu kuhusu usalama wa taarifa zao hasa baada ya muuzaji kuwa na uwezo wa kuifunga simu isitumike licha ya kwamba haipo katika himaya yake.

Vilevile, pamoja na sheria kukataza lakini kumekuwa na malalamiko kuhusu riba kubwa na masharti yasiyo ya wazi.

Isack Tarimo, Mkazi wa Sinza-Dar es Salaam, ambaye ni miongoni mwa waliokopa simu hizo, ameliambia Pambazuko kuwa wakopeshaji wengi hawatoi elimu kwa wateja wao kuhusu riba na masharti mengine.

"Hizi simu tunazikopa kwa vile tuna kipato kidogo. Kwa mfano sisi madereva wa bodaboda, hauwezi kuwa na laki mbili au tatu kwa wakati mmoja, ndio maana tunakimbilia huko kwenye mikopo..."

"Hata hivyo, ingawa inaonekana ni nafuu kukopa lakini ni mateso..."




"Mtu unalipa tu kila siku au kila wiki, kuna wakati hata hujui jumla umelipa kiasi gani maana hakuna uwazi," amesema.

Tarimo pia ameeleza wasiwasi wake kuhusu wakopeshaji wa simu hizo kuingilia mawasiliano yake.

"Mimi nimekopa tangu Januari na kwa siku narejesha Shilingi 2,700 nilichukua simu aina ya Infinix Smart 20 ambapo kwa fedha taslimu inauzwa Shilingi 380,000. Lakini nilipopiga hesabu nimebaini kuwa hadi nitakapomaliza deni nitakuwa nimelipa zaidi ya shilingi laki saba..."

"Kinachokera ni kwamba yaani ukichelewa tu kidogo kupeleka rejesho la siku unakuta simu imefungwa ghafla na huwezi kufanya chochote. Sasa kama wana uwezo wa kufanya haya hawawezi kuingilia mawasiliano yangu kweli?" anahoji.

Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Epoca), 2010; ambayo iko chini ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ndiyo sheria kuu inayolinda faragha ya taarifa za mteja, kuzuia matumizi mabaya ya huduma za simu na kuweka wajibu kwa kampuni za simu kuhakikisha usalama wa huduma.

Pia mwaka 2022, Bunge lilipitisha Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (The Personal Data Protrction Act, 2022), ambayo imeanza kutumika kulinda faragha na usalama wa taarifa za wananchi na inasimamiwa na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC).

Inaendelea Uk. 8

# Yaliyojificha nyuma

Inatoka Uk. 7

Kwa kuzingatia umuhimu wa sheria hizo, Pambazuko lilimtafuta Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma wa (TCRA), Rolf Kibaja, ambapo alisema mamlaka hiyo haihusiki na chochote kuhusu simu hizo za mikopo.

"TCRA haihusiki kabisa watafute watu wa taasisi inayohusika na taarifa binafsi… sisi kwenye simu hizo za mkopo hatuhusiki," amesisitiza Kibaja.

**Tume ya Ulinzi yanena**

Gazeti hili likamfikia Ofisa Habari wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Evelyne Urio, ambapo amesema hadi sasa hawajapata malalamiko yoyote kutoka kwa watumiaji wa simu hizo.

Pia amefafanua kuwa inategemeana na mikataba waliyokubaliana kati ya muuzaji na mtumiaji.

"Kwa mfano labda wamekubaliana kwamba mteja akikiuka masharti labda picha na details wanaziweka hadharani sasa kama waliandikishiana sisi hatuwezi kuingilia hilo..."

"Lakini kama anayekopesha kaenda kinyume na makubaliano sisi hapo ndio tunahusika na kumchukulia hatua," amesema.

Victoria Urassa, muuzaji wa simu hizo katika eneo la Kariakoo, akizungumzia utaratibu wa kumfungia simu mteja asipofanya marejesho, anasema kuna mfumo ambao wanauweka kwenye simu.



"Hata usipolipa ikipita ile tarehe automatically simu yenyewe inajifunga, yaani huwezi kufanya chochote," amefafanua.

Akielezea kuhusu hofu ya wateja kuwa wanaweza kuingiliwa faragha, Ahmed Khamis ambaye ni mkopeshaji wa simu hizo eneo la Makumbusho, anasema mfumo wa kukopesha unadhibiti uhuru wa simu kwa mtumiaji.

Anaongeza; "Jinsi mfumo ulivyowekwa simu yako huwezi kuifuta, lakini kuhusu kuingilia sijui kusoma meseji za mteja siyo kweli... wanahofu tu lakini hakuna kitu kama hicho."

**Lema aliwahi kusema**

Mbunge wa zamani wa Arusha Mjini, Godbles Lema (pichani), aliwahi kuandika kwenye ukurasa wake wa Instagram akisema wananchi wanadanganywa na wakopeshaji wa simu huku serikali ikiwa imekaa kimya.

"Mikopo ya simu imegeuka kuwa fataki kwa wananchi, Shilingi 100,000 zinakuwa Shilingi 240,000 kwa mwaka kutokana na takribani riba ya asilimia 20 kila mwezi…"

"Hii siyo mikopo bali ni kudanganya raia, inashangaza BoT imekaa kimya, ikiruhusu wananchi kuangamia kifedha kwa uzembe wao," aliandika Lema.

**BoT yawaonya**

Ofisa Itifaki na Uhusiano wa Umma wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Innocent Mmari, ameliambia Pambazuko kuwa mfumo wa ukopeshaji kwa simu unasimamiwa na BoT na kwamba mtoa huduma lazima awe amesajiliwa.

"Mtoa huduma lazima awe na leseni kutoka BoT kama Tier 2 Microfinance Service Provider na apate pia No Objection letter kabla ya kutoa huduma za mikopo,"amesema Mmari.

Hata hivyo, wakopeshaji simu kadhaa waliotembelewa na Pambazuko hawakutaka kuonyesha leseni hizo.

Alipoulizwa kama mikopo hiyo ni ya kidigitali, Mmari amesema: "Guidance Note inafafanua mkopo wa kidigitali kuwa mkopo ambao maombi, uidhinishaji, utoaji na marejesho yake yanafanyika kupitia njia za kidigitali kama vile simu ya mkononi, program (App), tovuti au majukwaa mengine ya kidigitali."

Kuhusu kikomo cha riba, amesema mwongozo unataka riba, ada, gharama zote, adhabu za kuchelewa kulipa, muda wa mkopo na masharti mengine yaonyeshwe wazi kwa mteja kabla hajachukua mkopo.

Katika hilo, akasisitiza kuwa mtoa huduma hawezi kubadilisha mfumo wa bei au gharama bila idhini ya BoT.

Inaendelea Uk. 9

# Yaliyojificha nyuma

Inatoka Uk. 8

Akizungumzia kuhusu ulinzi wa mteja, amesema mwongozo umeweka masharti ya kulinda taarifa binafsi za wateja kwa kuzingatia Sheria ya Ulinzi wa Taaifa Binafsi ya mwaka 2022.

"Kuzuia wakopeshaji kufikia contact list, sms, picha, email au taarifa nyingine zisizohitajika za mteja. "Kuzuia vitisho, unyanyasaji, aibu ya hadharani au kutuma ujumbe kwa ndugu na marafiki wa mteja kwa lengo la kumdhalilisha, kutaka taarifa za gharama za mkopo ziwekwe wazi, kuweka njia rasmi za kupokea malalamiko ya wateja," amesema alipotakiwa kutaja baadhi ya masharti hayo.

Kuhusu wauzaji wanaokwenda kinyume na sheria ya BoT, Mmari amesema wanachukuliwa hatua mbalimbali ikiwemo kusimamishwa kwa majukwaa yasiyo na leseni au yasiyotii maelekezo ya BoT.

"Hata wale ambao wanaendesha majukwaa bila No Objective Letter ya BoT nao tunawachukulia hatua kali," amesisitiza Mmari.

### Simu hazina ubora

Gazeti hili limebaini pia asilimia kubwa ya simu hizo kutokuwa na ubora ambapo mwanzoni mteja anaponunua inakuwa haina tatizo, lakini kadiri anavyotumia huwa inazimika mara kwa mara.

Josephat Eliud mkazi wa Makabe-Mbezi, ambaye ni miongoni mwa waliokopa simu hizo ameliambia Pambazuko kuwa wanapata changamoto kwani simu hizo zimekuwa hazina ubora.

"Mara nyingi wanatukopesha simu ambazo siyo nzuri huku nyingi zikiwa na matatizo. Simu unachukua leo baada ya siku chache tu inaanza kusumbua..." "Cha kusikitisha ni kwamba hata ukirudisha simu kwa ajili ya matengenezo, unaweza kuambiwa uiache hapo itengenezwe, halafu uchukue baada ya siku tatu au zaidi. "Hii inatuathiri sana kwa sababu simu ni kifaa muhimu kwa mawasiliano na shughuli zetu za kila siku," amesema.

Amesema mbali na matatizo hayo, gharama wanazotozwa ni kubwa sana, hivyo wanahisi kuna udanganyifu au ukosefu wa uwazi. Kutokana na hilo, ameiomba mamlaka husika kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini ukweli na kulinda haki za wateja.

### Maduka ya 'cash' hoi

Katika ufuatiliaji wake Pambazuko limebaini kuwa wafanyabiashara wanaouza simu kwa pesa taslimu sasa hawapati wateja wengi kwani wateja wengi wanakimbilia kwenye simu za mikopo.

Wachumi waliozungumza na Pambazuko wamesema hilo linatokana na ugumu wa hali ya maisha.

"Mtu anaona afadhali alipe simu kidogo kidogo kwani hana fedha nyingi taslimu za kununua simu. Hata akijua kuwa mwishowe atalipa fedha mara dufu lakini kule kulipa kidogo kidogo kunampa nafuu kwa sababu kipato chake ni kidogo,: anasema mchumi mmoja.

Wakizungumza na Pambazuko kwa nyakati tofauti wafanyabiashara hao wa simu wamesema tangu biashara ya simu za mikopo zilipoanza wamekuwa na hali mbaya.

"Yaani unaweza kukuta siku nzima nimepata mteja mmoja au kuna wakati hakuna hata mmoja, imefika hatua wenzangu wengine imebidi na wao waanze kuuza kwa mikopo.

"Mimi hapa nimeajiriwa lakini naona dalili ya bosi kufunga duka maana hali ni mbaya," amesema Pendo Cosmas, anayeuza duka la simu eneo la Mwenge.

### Kelele za matangazo

Changamoto nyingine ambayo gazeti hili limebaini ni kelele za spika zinazoshindana kutangaza biashara hiyo ya kukopesha simu.

Baadhi ya maeneo yenye misongamano ambayo yameshamiri kwa kelele za spika katika Jiji la Dar es Salaam ni Kariakoo, Mwenge, Manzese, Makumbusho, Bunju B na Tegeta.

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limewahi kueleza kuwa vyanzo vya kelele mijini vinahitaji kudhibitiwa kupitia matumzi sahihi ya ardhi, vibali kutoka mamlaka husika na matumizi ya vifaa vya kudhibiti sauti.

Changamoto za kelele, inasimamiwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Kanuni za Udhibiti wa Kelele na Mitetemo za mwaka 2015.

Sheria hiyo inapiga marufuku uzalishaji wa sauti kubwa zinazozidi viwango vinavyoruhusiwa katika maeneo ya makazi, biashara, karibu na taasisi za kijamii.



Tafakuri ya Bagonza

Na Dkt. Benson BAGONZA

# Haya yalikuwa makosa ya kimkakati, yamepokonya fursa!

TAIFA linahitaji maridhiano. Yawe ya kweli au ya hila, ni muhimu kutambua makosa matatu ya kimkakati yaliyotupokonya fursa na sifa nzuri ya taifa letu.

Haya ndiyo makosa ya kujutia iwe kwa uwazi au kwa siri.

Mosi, kumfunga Freeman Mbowe – aliyekuwa Mwenyekiti wa Chadema kwa miezi minane kulitoa mwanya kwa wanasiasa wenye misimamo mikali kukiteka chama.



Watu kama Tundu Lissu, Godbless Lema, Joseph Mbilinyi (Sugu), John Heche, Peter Msigwa, Ezekiel Wenje na wengine, walijiimarisha kwenye chama wakati Mbowe yuko gerezani.

CCM na serikali wakakosa mtu wa "kuridhiana" naye kwa sababu aliyekuwa akiwasaidia walimweka gerezani. Alipoachiwa, chama kiliishaenda mikononi mwa wenye msimamo mkali.

Mbowe aliwahi kuionya serikali lakini haikujali. Aliyeshauri Mbowe awekwe ndani, shetani anamuona.

Pili, kukataa maridhiano kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 2025 lilikuwa kosa jingine ambapo wanasiasa wenye msimamo mkali ndani ya CCM walikataa maridhiano kabla ya uchaguzi.

Wangeweza kwenda mezani na "kuwatuliza" wenye msimamo mkali kule Chadema na kuwaingiza kwenye uchaguzi, halafu goli la mkono lisingekomba kila kitu, bali lingeacha masalia ya wabunge na madiwani.

Kwa CCM kukataa maridhiano kukawafanya wenye msimamo mkali ndani ya Chadema kugomea uchaguzi. Kilichotokea Oktoba 29 kingeepukwa kama CCM ingekubali maridhiano. Kukataa maridhiano lilikuwa kosa kubwa la kimkakati.

Tatu, kumweka ndani Tundu Lissu lilikuwa kosa jingine la kimkakati ambapo wenye misimamo mikali ndani ya CCM na mfumo walishinikiza Lissu akamatwe na kufunguliwa kesi mbaya.

Hatua hii ikaiongeza vuguvugu ndani ya Chadema na pia hatua hii ikaigawa hata CCM, jumuia ya kimataifa, hata na taasisi nyeti zenye utakatifu fulani ndani na nje ya serikali.

Utekaji wa wana CCM na wapinzani, ukafunga uwezekano wa maridhiano. Kwa mara ya kwanza, hata viongozi wakuu "wakaonekana" kupoteza mwelekeo na kuwa wenye msimamo mkali. Badala ya maridhiano wakaanza kuimba "kujisalimisha tu!"

Mpaka hapa tukubaliane. Tulimfunga Mbowe, wenye msimamo mkali wakachukua chama. Tumemfunga Lissu, chama chote kimekuwa na wakubwa wenye misimamo mikali. Kuwekana ndani siyo dawa nzuri ya kushughulikia upinzani.

Makosa haya matatu ya kimkakati yameifanya nchi ionekane imejiteka, imejifunga pingu na kupoteza funguo.

Fursa nyingi za kumaliza jambo hili kisiasa zimepotea. Mahakama zinateseka kulimaliza huku zimefungwa au kujifunga pingu mikononi na miguuni.

Chadema ina misimamo mikali. CCM ina misimamo mikali na jeuri. Mbowe alipokuwa madarakani alidhalilishwa na CCM mpaka Chadema ikamweka chini. Sasa dola inamwona Mbowe wa maana wakati ni yenyewe ilimwangusha?! Chadema sasa inamzodoa aliyekuwa mwamba wao. Mwe! Bora ukose akiba ya chakula, lakini uwe na akiba ya maneno.

Kama hayati Edward Lowassa, alichafuliwa na kusafishwa na vyama vyote CCM na Chadema. Alikufa akiwa mshindi kwa vyote.

Wazee wa Kikurya husema "Mdharau mwiba..", lakini wajanja wa Kijaluo wao husema, "unaweza kudharau siafu, lakini usiwakalie kwa makalio yasiyo na kinga".

Ni muda sasa wa kuwatoa watu magerezani, nasi tujitoe gerezani. Turudi mezani bila hila wala aibu.

***Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.***



Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA

Kona ya Dkt. Bisimba

# Siku ya Ubinadamu Duniani ina maana halisi kwa watu?

KATIKA mlolongo wa siku zinazoazimishwa kidunia, ipo siku ya Kimataifa ya Ubinadamu (World Humanitarian Day), ambayo huadhimishwa Agosti 19 kila mwaka.

Siku hii hutumika kuwakumbuka na kuwaheshimu watu wanaojitoa kuwasaidia wengine walio katika mazingira magumu, wakati mwingi wakihatarisha maisha yao wenyewe.

Katika siku hii, watu wote wanaalikwa kutafakari iwapo bado tunauona ubinadamu wa mwingine. Unamuangaliaje mtu mwingine katika mazingira yoyote yale aliyonayo?

Siku hii ilianzishwa ikihusishwa na tukio la kusikitisha sana lililotokea Baghdad, Iraq mnamo Agosti 19, 2003.

Katika siku hii lilitokea shambulio la bomu katika makao ya Umoja wa Mataifa na waliuawa watu 22 waliokuwa wakifanya kazi za kibinadamu kwa kuwasaidia waathirika wa vita.

Kati ya waliouawa ni Sergio Vieira de Mello, aliyekuwa mwakilishi maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa nchini Iraq.

Hii ni siku muhimu iliyowekwa kukumbuka madhila hayo ya maisha yaliyopotea kwa ajili ya kuwahudumia wengine.

Ni siku ya kutambua ujasiri wa maelfu ya watu duniani wanaofanya kazi za kibinadamu wakati wa vita, majanga, njaa, magonjwa na misiba mbalimbali.

Tunapoitazama siku hii kwa jicho pana zaidi tunaona kwamba ubinadamu siyo jukumu la mashirika ya misaada pekee.

Ubinadamu unaanza pale tunapoweza kumuona binadamu mwingine kama mwanadamu mwenye utu, heshima na haki kama sisi wenyewe.

Mtu anapokumbwa na janga, mtoto kuteseka, mtu mwenye ulemavu kukosewa fursa, familia inapopoteza makazi au tunapoona mtu ananyanyaswa kwa sababu yoyote ile, swali kwetu tunaoona siyo tu kwamba ‘nani anapaswa kumsaidia, bali tujihoji kama jamii tunafanya nini?

Nimekumbuka kisa kilichotokea kwenye eneo la mahakama moja Dar es Salaam, ambapo askari walikuwa wanamshambulia raia mmoja kwa mateke na virungu na wapo watu wengi wamezunguka hapo wakiangalia.

Baadaye akatokea mwanadada mmoja, akaamua kumvuta yule aliyekuwa anapigwa bila kujifikiria kuwa naye yangeweza kumkuta kama ya huyo aliyekuwa anashambuliwa.

Huo ndiyo mfano mdogo wa ubinadamu.

Ubinadamu unahitaji huruma, lakini huruma pekee haitoshi, unahitaji zaidi ni kuheshimu haki na utu wa mwingine katika sehemu yoyote ulipo kama binadamu, uwe kiongozi, uwe mtendaji katika dola au hata mhudumu katika taasisi.

Usidhani kuwa ni lazima msaada mkubwa ni kumpatia mtu fedha, au chakula, bali ukiweza kumsikiliza, kumlinda mtu dhidi ya manyanyaso, kumtetea anaponyimwa haki yake au hata kumpa nafasi ya kusimama kwa miguu yake mwenyewe.

Tunapoitazama dunia iliyojaa migogoro, chuki na tofauti zinazotugawa kama binadamu, siku hii ya kimataifa ya ubinadamu inatukumbusha jambo moja muhimu, maumivu ya mwanadamu mwenzako hayapaswi kuwa jambo lisilokuhusu.

Hata nasi Watanzania kwa hali tuliyonayo nchini kipindi hiki tunahitaji kujihoji tunawachukuliaje watu walio katika dhiki mbalimbali ikiwa ni pamoja na kudhulumiwa, kupotelewa na ndugu kwa njia zisizoeleweka.

Je, tunawapa usaidizi wowote hata kama ni wakuwafariji tu? Tumewahi kusimama dhidi ya dhulma na kuonewa kwa mwingine?

Ujumbe mkubwa wa siku hii si kuwasaidia wengine pekee ni kukumbusha kuwa na ubinadamu kwa binadamu wenzetu.

Tunaposhindwa kuuona ubinadamu wa mwingine tunakuwa katika hatari ya kupoteza sehemu ya ubinadamu wetu wenyewe.

***Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.***

Habari

# Mawakili kupambana kumnasua Rais Samia Kesi ya Lissu



*Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu, akipitia nyaraka muhimu kabla ya kuanza kuwasilisha utetezi wake mbele ya majaji wanaosikiliza kesi ya uhaini inayomkabili katika Mahakama Kuu, Masjala ndogo ya Dar es Salaam juzi. Na leo anaendelea na utetezi. (Picha na Pambazuko).*

**Na Mwandishi WETU**

MWENYEKITI wa Chadema, Tundu Lissu leo anatarajiwa kuendelea kujitetea katika kesi ya uhaini inayosikilizwa katika Mahakama Kuu - Masjala Ndogo ya Dar es Salaam.

Katika hatua ya sasa, mawakili wa serikali wanaingia katika mtihani wa kumnasua Rais Samia Suluhu Hassan kuitwa mahakamani baada ya majaji kutoa uamuzi kuwa Lissu ana kesi ya kujibu.

Lissu anayekabiliwa na kesi ya uhaini namba 19605/2025 alianza utetezi wake Ijumaa iliyopita, Agosti 21, 2021 ikiwa ni mwendelezo wa kesi hiyo iliyodumu kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa.

Katika uamuzi wa Ijumaa iliyopita, jopo la majaji watatu wanaosikiliza kesi hiyo wakiongozwa na Jaji Dunstan Ndunguru, liliamua Lissu ana kesi ya kujibu katika kesi hiyo ya uhaini inayomkabili, hatua inayofungua njia kwa mwanasiasa huyo kuanza kujitetea. Majaji wengine ni James Karayemaha na Ferdinand Kiwonde.

Baada ya uamuzi wa mahakama, Lissu alisema atajitetea akiwa shahidi wa kwanza na kuomba mahakama iwaite mashahidi wengine alioeleza kuwa ni muhimu ambao ni pamoja na Rais Samia Hassan, watendaji wa vyombo vya dola na viongozi wakuu wastaafu.

Lissu alitaja mashahidi wengine kuwa ni Dkt. Phillip Mpango, aliyekuwa makamu wa rais, Kassim Majaliwa, aliyekuwa waziri mkuu, Jenerali Jacob Mkunda, mkuu wa majeshi ya ulinzi, Camillus Wambura, mkuu wa jeshi la polisi (IGP), Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Ramadhani Kingai, Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa, Suleiman Mombo na Kamishna wa Polisi (DCP) Ramadhani Ng'anzi.

Pia aliwataja wanaharakati kutoka nchi za Afrika Mashariki ambao ni Agather Atuhaire, Boniface Mwangi, Dkt Willy Mutunga, Martha Karua, wamahabari John Marwa, na viongozi wa Chadema ambao ni Amani Golugwa, John Heche na John Mnyika.

Mchuano mkubwa uliibuka mahakamani hapo Ijumaa iliyopita, baada ya kiongozi wa jopo la mawakili wa serikali - wakili wa serikali mkuu, Nassor Katuga kupinga kuitwa kwa Rais Samia mahakamani ambapo alieleza kuwa kwa nafasi yake, mashahidi waliotoa ushahidi ambao ni wasaidizi wake walishawasilisha ushahidi wao mahakamani.

Alisema msingi wake unajengwa katika mantiki kwamba mtumishi yeyote wa serikali anatekeleza shughuli zake kwa niaba ya na kwamba rais ndiye kiongozi wa serikali, hivyo mashahidi waliotoa ushahidi walifanya hivyo kwa niaba ya rais.

Katuga alitaka ihesabike kuwa kupitia wao, kwa maneno mengine, rais ameshatoa ushahidi pamoja na wengine waliokuwa wasaidizi wake, akiwemo aliyekuwa makamu wake na waziri mkuu wake.

Inaendelea Uk. 13

# Mawakili kupambana

Inatoka Uk. 12

"Kwa hiyo hakuna haja ya kuwaita mashahidi hao ambao kwa kuwa ushahidi wao umeshatolewa na watumishi wa serikali, ni kama vile anataka hawa wafike ili afanye cross examination (awafanyie mahojiano) ya kile kilichoelezwa na mashahidi hao," alisema.

Pia alisema hoja yake inasimama katika msingi mkuu wa kifungu cha nane cha Sheria ya Ulinzi wa Rais (Presidential Affairs Act) kinachoainisha kinga mbili kuu za kisheria kwa mkuu wa nchi.

Kinga hizo ni dhidi ya kukamatwa kwamba rais aliyeko madarakani hawezi kukamatwa wala kuzuiliwa chini ya sheria yoyote na kinga ya kutofika mahakamani, kwamba hakuna amri ya mahakama au wito wa kisheria unaoweza kumlazimisha Rais kufika mahakamani kibinafsi wakati anatumikia muhula wake.

Hoja hizo zilipingwa vikali na Lissu ambaye alisema tuhuma dhidi yake zinamhusu moja kwa moja rais ambaye ndiye mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama pamoja na wasaidizi wake, makamu na waziri mkuu ambao wote ni wajumbe wa baraza hilo.

Alisema tuhuma za uhaini ni nzito na zinazohusu tishio la usalama kwa taifa, hivyo mwenyekiti wa baraza la usalama la taifa ni lazima awepo ili kuthibitisha uwepo wa tishio hilo.

Lissu alieleza kuwa iwapo kuna hoja kwamba rais hawezi kufikishiwa wito moja kwa moja, utaratibu unaeleza wazi kuwa anaweza kufikishiwa wito huo kupitia kwa katibu mkuu kiongozi au kupitia kwa katibu wake binafsi, bila kujali kama ataupuuza au laa.

Mvutano baina ya pande hizo mbili unatarajiwa kuendelea katika utetezi wa Lissu unaotarajiwa kuendelea leo, wakati kesi hiyo itakapoendelea kusikilizwa.

Katika kesi hiyo, Lissu alikamatwa Aprili 9, 2025 muda mfupi baada ya kuhutubia mkutano wa chama chake, Chadema mjini Mbinga, kusini mwa Tanzania, ambapo siku iliyofuata, Aprili 10, 2025, alifikishwa katika mahakama ya hakimu mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam.

Alishtakiwa kwa kosa la uhaini, pamoja na shtaka jingine la kuchapisha taarifa zinazodaiwa kuwa za uongo. Shtaka la uhaini ni miongoni mwa makosa mazito zaidi katika sheria za Tanzania.

Upande wa mashtaka uliwasilisha mashahidi 17 ambao baada ya kumaliza kuwasilisha ushahidi wake, mahakama ilitoa uamuzi kwamba ushahidi huo unatosha kumtaka Lissu ajitetee, kwa kuwa amekutwa na "kesi ya kujibu".

"Mahakama imeamua kwamba upande wa mashtaka umejenga kesi ambayo mshtakiwa anapaswa kuijibu," alileza Jaji Ndunguru wakati akitoa uamuzi huo Ijumaa iliyopita.

Jaji Ndunguru alieleza kuwa mahakama ilifikia uamuzi huo baada ya kuchunguza ushahidi uliowasilishwa na upande wa mashtaka pamoja na hoja za Lissu, ambaye aliiomba iachilie mbali kesi hiyo kwa madai kwamba hakuna ushahidi wa msingi unaomhusisha na kosa la uhaini.

Inaendelea Uk. 14



*Makamu Mwenyekiti wa Chadema, John Heche (kushoto), akiwa na Mwenyekiti wa Kanda ya Pwani, Boniface Jacob wakati wa kesi ya uhaini inayomkabili Tundu Lissu katika Mahakama Kuu, Masjala ndogo ya Dar es Salaam juzi. (Picha na Pambazuko).*

■ Habari

# Mawakili kupambana

Inatoka Uk. 13

Jaji Ndunguru alisema jukumu la mahakama katika hatua hiyo lilikuwa kuamua ikiwa ushahidi wa upande wa mashtaka, endapo hautapingwa, unaweza kutosha kumtia mshtakiwa hatiani.

Alisema mahakama haikuhitajika kufanya uchambuzi wa kina kuhusu uzito au uaminifu wa kila ushahidi katika hatua hiyo na masuala hayo yatazingatiwa baada ya Lissu kuwasilisha utetezi wake.

Kwa mujibu wa mahakama, ushahidi uliotolewa na mashahidi wa upande wa mashtaka ulimhusisha Lissu kwa kiwango kinachotosha na matamshi yaliyowekwa katika hati ya shtaka.

Upande wa mashtaka uliita mashahidi 17 kati ya 30 waliokuwa wameorodheshwa kabla ya kufunga ushahidi wake Agosti 17, ambapo waendesha mashtaka waliiambia mahakama kwamba ushahidi huo ulitosha kuthibitisha hoja muhimu za shtaka na kumtaka Lissu ajitetee.

Lissu anakabiliwa na shtaka moja la uhaini chini ya Kifungu cha 39(2)(d) cha Kanuni ya Adhabu ya Tanzania, kutokana na matamshi anayodaiwa kutoa Aprili 3, 2025, katika mkutano uliofanyika katika makao makuu ya Chadema jijini Dar es Salaam.

Upande wa mashtaka unadai kwamba matamshi hayo yalihusiana na msimamo wa Chadema wa kutoshiriki katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 bila kufanyika kwa mageuzi ya mfumo wa uchaguzi.

Waendesha mashtaka wanadai kwamba Lissu alihamasisha wananchi kuzuia uchaguzi huo na kutoa matamshi yaliyokusudiwa kuishinikiza na kuitishia serikali.




*Stendi mpya ya daladala inayojengwa eneo la Mbezi, Dar es Salaam ambayo ilikuwa iwe mbadala wa stendi ya zamani, sasa imegeuzwa maegesho ya maroli kama ilivyokutwa na kamera ya Pambazuko jana.*

# Serikali yachunguza CT-Scan Aga Khan

Na Waandishi WETU



SERIKALI kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA), imeanza uchunguzi wa tukio la kulipuka kwa mashine ya kitabibu inayotumia miale ya Xray na teknolojia ya kompyuta kupiga picha ndani ya mwili wa binadamu (CT-Scan), kwenye Hospitali ya Aga Khan ya mjini Dar es Salaam.

Hatua hiyo inakuja wiki moja tu baada ya gazeti hili kufichua kadhia hiyo wiki iliyopita kwa CT-Scan kulipuka ikiwa na mgonjwa akifanyiwa uchunguzi.

Kufuatia tukio hilo, mgonjwa aliandika barua ya madai kupitia wanasheria wake, akitaka kulipwa fidia ya Shilingi milioni 350 na hospitali hiyo kubwa nchini kutokana na kudai kusababishiwa tatizo la kupumua ambalo hakuwa nalo awali.

Barua hiyo ambayo Pambazuko imeiona, ikiwa na kumbukumbu AVL/BR/2026/07/14/01, ya Julai 14, 2026, inadai kuwa fedha hizo ni fidia ya jumla kwa maumivu, mateso, msongo wa mawazo, matatizo ya kisaikolojia, mshtuko, usumbufu na hasara alizozipata kutokana na uzembe wakati akifanyiwa kipimo cha CT- Scan.

Aidha, hospitali hiyo imetakiwa kutoa dhamana ya maandishi ya kukubali kuwajibika na kugharamia gharama zote za matibabu ya sasa na yajayo, madeni na matatizo ya kiafya yatakayothibitika kuwa yametokana moja kwa moja na tukio hilo.

Taarifa zilizolifikia gazeti hili zinabainisha kuwa baada ya kuchapishwa kwa habari hiyo, maofisa wa TMDA walifuatilia suala hilo, lakini uongozi wa hospitali uliwahakikishia kuwa mashine yao ya CT-Scan na vifaa tiba vingine viko imara na havina tatizo lolote.

Meneja wa Ufuatiliaji Usalama wa Vifaa Tiba na Vitendanishi wa TMDA, David Matle, amelithibitishia gazeti hili kuwa mamlaka hiyo inalifuatilia suala hilo ili kujua ubora wa kifaa hicho.

TMDA ndio taasisi yenye mamlaka ya kudhibiti ubora wa vifaa tiba nchini.

Tukio la mashine hiyo kulipuka ikiwa na mgonjwa ndani lilitokea Juni 4, mwaka huu hospitalini hapo wakati mgonjwa ambaye ni mwanafunzi wa chuo cha teknolojia Dar es Salaam (DIT), akifanyiwa uchunguzi.

Taarifa zinaeleza kuwa, kijana huyo mwenye umri wa miaka 20, alifikishwa hospitalini hapo Juni 3, mwaka huu akikabiliwa na maumivu makali ya mwili, hivyo madaktari kuamua kumfanyia uchunguzi kwa kipimo cha ST-Scan.

Hadi leo wakati Pambazuko inachapisha habari hii, zimebaki siku tatu kumalizika muda ambao wanasheria hao wameipa Hospitali ya Aga Khan, kulipa madai ya mteja wao.

Wanasheria hao pia wanaitaka hospitali hiyo kutoa dhamana ya maandishi ya kukubali kuwajibika na kugharamia gharama zote za matibabu ya sasa na yajayo, madeni na matatizo ya kiafya yatakayothibitika kuwa yametokana moja kwa moja na tukio hilo.

Wanasheria hao wameonya kuwa endapo Hospitali ya Aga Khan itashindwa, itapuuza au kukataa kutekeleza madai hayo ndani ya muda uliowekwa, watachukua hatua za kisheria bila kutoa taarifa nyingine kwao.

■ Habari

# THRDC: Haki, suluhu kesi ya Lissu viharakishwe



Na Mwandishi WETU

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), umetoa mapendekezo kuhusu hatma ya kesi inayomkabili Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu, ukitaka hatua zichukuliwe haraka kuimarisha haki, utawala wa sheria na maridhiano ya kitaifa.

Lissu anakabiliwa na shtaka moja la uhaini kinyume na kifungu cha 39(2) (d) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, linalotokana na maneno aliyoyatamka kuhusiana na kusudio la kuzuia kufanyika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Katika tamko lao, THRDC imeiomba Mahakama kuhakikisha shauri hilo linasikilizwa na kuamuliwa kwa haraka, kupunguza ucheleweshaji na kusimamia kwa umakini maombi ya kuahirisha kesi.

Akizungumza na waandishi wa habari wiki iliyopita, Mratibu wa Taifa wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, amesema mapendekezo hayo yametokana na ufuatiliaji wa mwenendo wa kesi hiyo uliofanywa na mtandao huo.

"Tunaitaka serikali kutumia mifumo ya kisheria iliyopo, ikiwemo mamlaka ya DPP inapofaa, kutafuta suluhisho la shauri la Lissu kwa kuzingatia haki, umoja wa kitaifa na mshikamano wa kijamii,"amesema Olengurumwa.

Olengurumwa amesema mazungumzo na maridhiano ni muhimu katika kutatua changamoto, ikiwemo suala la Katiba Mpya.

Pia amesema katika uchambuzi wake mtandao huo ulibaini changamoto kadhaa katika mwenendo wa kesi hiyo inayomkabili Lissu baada ya kufanya ufuatiliaji kuanzia Aprili 9, 2025 hadi Agosti 19, 2026. Olengurumwa amesema timu ya ufuatiliaji wa awali ukiongozwa na Mkuu wa Idara ya Utetezi wa THRDC, Paul Kisabo, imesema ufuatiliaji huo ulihusisha hatua mbalimbali za mchakato wa haki jinai, ikiwemo kukamatwa na kufikishwa mahakamani.

Pia mazingira ya kizuizini, upatikanaji wa uwakilishi wa kisheria, mawasiliano na familia, ushiriki wa umma na waangalizi, mwenendo wa upande wa mashtaka pamoja na kuahirishwa kwa kesi.

THRDC imesema ilibaini kuwa Lissu alipokamatwa Mbinga mkoani Ruvuma Aprili 9, 2025, hakuelezwa sababu za kukamatwa kwake wakati huo wala alipokuwa akisafirishwa hadi Dar es Salaam.

"Alijulishwa mashtaka baada ya kufikishwa Kituo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam Aprili 10, 2025…"

"Akafikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu siku moja baada ya kukamatwa, ambapo shtaka la uhaini lilisomwa na kufafanuliwa kwake, ingawa hakutakiwa kujibu kwa kuwa mahakama hiyo haikuwa na mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo,"amesema Olengurumwa.

Inaendelea Uk. 17

# THRDC: Haki, suluhu

Inatoka Uk. 16

Vilevile Olengurumwa amesema Lissu ameendelea kuwa mahabusu kwa muda mrefu kutokana na uhaini kutokuwa kosa linalodhaminika, hali ambayo imeibua hoja kuhusu haki ya uhuru, dhana ya kutokuwa na hatia na haki ya kusikilizwa ndani ya muda unaofaa.

Akifafanunua zaidi mratibu huyo amesema, wamebaini changamoto katika mazingira ya kizuizini na uendeshaji wa kesi ya uhaini inayomkabili Lissu.

"Changamoto ilijitokeza baada ya Lissu kuhamishwa kutoka Gereza la Keko kwenda Ukonga bila wawakilishi wake wa kisheria au wanafamilia kupewa taarifa kabla jambo ambalo ni kosa kisheria.

"Pia tulipokea taarifa kuwa baadhi ya mipangilio ya kiusalama inayotumika kwa wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kifo ilitumika kwa Lissu ambaye hajatiwa hatiani.

"Pia imetaja vikwazo vya kutembelewa na familia, kupata taarifa na kushiriki ibada za kidini akiwa kizuizini,"amesema Olengurumwa.

Kuhusu uwakilishi wa kisheria, Olengurumwa amesema wamebaini changamoto katika mawasiliano ya siri kati ya Lissu na mawakili wake. Kwamba baadhi ya mashauriano yaliwekewa muda mfupi au kufanyika katika mazingira ambayo hayakuhakikisha usiri wa kutosha.

"Wawakilishi wa Lissu walikumbana na vikwazo vya kumfikia mteja wao. Ilipokea taarifa kuwa nyaraka na mawasiliano ya kisheria yalikaguliwa kabla ya kumfikia mshtakiwa,"amesema.

Katika eneo la ushiriki wa umma, amesema waandishi wa habari, wafuasi, wanaharakati na wananchi walikumbana na vikwazo vya kuhudhuria baadhi ya vikao vya kesi.

Ameeleza kuwa baadhi ya waangalizi wa kikanda na kimataifa walizuiwa kufuatilia mashauri, huku kukiwa na uwepo mkubwa wa vikosi vya usalama ndani na nje ya mahakama.

Olengurumwa amesema ucheleweshaji wa kesi hiyo unaibua hoja kuhusu haki ya kusikilizwa kwa kesi ndani ya muda unaofaa, hasa kwa kuwa Lissu ameendelea kuwa kizuizini.

Kwa upande wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), amesema wanapendekeza kutathmini utoshelevu wa ushahidi unaotumika kuendesha mashtaka na kuhakikisha maamuzi yanaongozwa na maslahi ya haki na umma.

Kuhusu Jeshi la Magereza, Olengurumwa amesema THRDC imependekeza mahabusu watendewe kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa, wapewe fursa ya kuonana na familia, kupata nyaraka za kisheria na huduma muhimu, pamoja na kushiriki ibada bila ubaguzi.




*Rais Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri, Dkt. Mostafa Kamal Madbouly na viongozi wengine wakipiga kofi baada ya kuzindua mitambo tisa ya kuzalisha umeme wa megawati 2,115 ndani ya jengo la mitambo (Power House) katika Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Julius Nyerere (JNHPP), Rufiji mkoani Pwani juzi. (Picha zote na Ikulu).*





# Viwanda vya baruti kupunguza uagizaji nje

Na Mwandishi WETU

MKOA wa Pwani umeendelea kujijenga kuwa kitovu cha uchumi Tanzania na sasa imeingia kwenye viwanda vinavyozalisha bidhaa muhimu katika sekta ya madini.

Pwani sasa imeingia katika uzalishaji wa baruti na vilipuzi, bidhaa ambazo hutumika kwenye shughuli za uchimbaji madini, lakini hazizalishwi kwa wingi nchini.

Taarifa iliyotolewa wiki iliyopita inaeleza kuwa viwanda viwili vya baruti na vilipuzi vinajengwa katika wilaya ya Kisarawe mkoani humo.

Ujenzi wake utakapokamilika viwanda hivyo vitaongeza kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa bidhaa hizo ndani ya nchi na kupunguza uagizaji wake nje ya nchi.

Viwanda hivyo vimetajwa kuwa ni Ideal Detonators Tanzania Limited, kinachotarajiwa kuwa miongoni mwa viwanda vikubwa vya aina hiyo katika ukanda wa Afrika Mashariki, na Solar Intracom Chemicals Limited.

Kiwanda cha Ideal kina uwezo wa kuzalisha tani 84,000 za baruti na vipande 50,000 vya vilipuzi kwa mwaka, huku kiwanda cha Solar kikiwa na uwezo wa kuzalisha tani 25,000 za baruti na vipande 15,000 vya vilipuzi kwa mwaka.

Akizungumza wakati wa ziara aliyoifanya wilayani Kisarawe wiki iliyopita, Naibu Waziri wa Madini, Dkt. Steven Kiruswa, alisema uwepo wa viwanda hivyo utasaidia kuongeza upatikanaji wa baruti na vilipuzi vinavyohitajika katika shughuli za migodi na matumizi mengine nchini.

Katika ziara hiyo, naibu waziri huyo alikuwa akikagua na kuangalia shughuli za madini, kufahamu changamoto za wawekezaji na kufuatilia utekelezaji wa miradi mbalimbali iliyo chini ya wizara hiyo.

Dkt. Kiruswa alisema mahitaji ya baruti nchini yanakadiriwa kufikia wastani wa tani 79,548.22 kwa mwaka.

Inaendelea Uk. 19



# Viwanda vya baruti

Inatoka Uk. 18

Aidha, kwa upande wa vilipuzi, alisema mahitaji yapo kwenye vipande 29,663.17 kwa mwaka hivyo uwekezaji huo ni muhimu kwa kuwa utaongeza uzalishaji wa ndani wa bidhaa hizo.

Dkt. Kiruswa alisema uwekezaji huo unaonesha utekelezaji wa dhana ya uongezaji thamani madini, kwa kuwa Tanzania inalenga siyo tu kuchimba madini, bali pia kuzalisha bidhaa kutokana na madini hayo yanayochimbwa nchini.

"Baruti ni miongoni mwa bidhaa muhimu katika shughuli za uchimbaji madini, kwani huwezesha wachimbaji kuyafikia madini…"

"Uzalishaji wa bidhaa hizi hapa nchini utaongeza upatikanaji wake na kupunguza utegemezi wa uagizaji bidhaa kutoka nje," alisema Dkt. Kiruswa.

Kuhusu changamoto ya soko la ndani iliyowasilishwa na Solar Intracom Chemicals, Dkt. Kiruswa alisema wizara inalichukua suala hilo kwa uzito na italishughulikia kwa kushirikiana na wadau, ili kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa nchini zinapata soko na viwanda vinaendelea kuzalisha.

Alisema ikiwa serikali imeweza kushughulikia changamoto zilizowahi kujitokeza katika sekta nyingine za uzalishaji ikiwemo chumvi, hivyo ina imani kuwa changamoto zinazokabili uzalishaji wa baruti na vilipuzi nazo zitapatiwa ufumbuzi.

### Udhibiti

Uzalishaji wa vilipuzi nchini siyo shughuli ya kawaida ya viwanda. Chini ya sheria ya vilipuzi sura ya 45, mtu haruhusiwi kutengeneza vilipuzi bila kuwa na leseni au kibali halali.

Sheria pia inadhibiti uagizaji, usafirishaji, uuzaji, umiliki, uhifadhi na matumizi ya vilipuzi.

Aidha, kanuni za sheria hii za mwaka 2019 zinaweka masharti maalumu kwa viwanda vya vilipuzi, yakiwemo mahitaji ya kupata idhini kabla ya ujenzi, hatua za usalama, ulinzi wa malighafi na bidhaa, mafunzo ya Watanzania, utunzaji wa kumbukumbu na utoaji wa taarifa za uzalishaji kila mwezi.



Tume ya Madini pia inaeleza kuwa mwombaji wa leseni ya kutengeneza vilipuzi anatakiwa kuwasilisha michoro na mpangilio wa kiwanda, barua kutoka kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, kufanyiwa ukaguzi na Tume ya Madini kabla na baada ya ujenzi, pamoja na kupata maoni ya Firearms and Ammunition Control National Committee.

### Kwa mtazamo wa biashara

Hili ni eneo lenye fursa kubwa lakini lenye vizingiti vikubwa vya kuingia. Mahitaji yake yanaendeshwa zaidi na ukuaji wa sekta ya madini, ujenzi wa miundombinu na uchimbaji wa mawe.

Kwa Tanzania inayolenga kuongeza uzalishaji wa madini na kuongeza thamani ndani ya nchi, uzalishaji wa vilipuzi ni sehemu muhimu ya kukuza uzalishaji wa ndani katika mnyororo wa thamani wa madini.

Habari

# Wasira ahimiza vikao CCM, kujitambua



Na Mwandishi WETU, Singida

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Stephen Wasira, amewataka wanachama wa chama hicho kukutana mara kwa mara katika vikao rasmi.

Amehimiza vikao vya chama chao ili kujadili masuala muhimu na kuepuka kupotoshwa na taarifa zisizo na ukweli zinazosambazwa kwenye mitandao ya kijamii.

Akizungumza wiki iliyopita katika ziara yake wilayani Ikungi, Singida Wasira alisema vikao hivyo vinawapa wanachama fursa ya kupata taarifa sahihi na kuambizana ukweli.

“Wanachama wetu nchi nzima, kwa mujibu wa Katiba mna vikao vya wanachama. Mkutane muambizane. Siku hizi kwenye mitandao kuna uongo mwingi sana. Usipoangalia unaweza hata wewe kushirikishwa kusema uongo,” alisema.

Alisisitiza kuwa ni muhimu wanachama kukutana na kujadili madai yanayosambaa, kisha kumtafuta mtu mwenye ujuzi awasaidie kuyafafanua na kuujua ukweli.

Makamu Mwenyekiti huyo alibainisha kuwa mikutano ya wanachama ni fursa muhimu ya kujadili masuala yanayoendelea nchini ili waweze kukitetea chama ipasavyo.

Kuhusu uhuru na umoja wa nchi, Wasira amesema CCM itaendelea kulinda urithi huo uliopatikana kwa kazi kubwa.

Aliongeza kuwa wapo wanaodai CCM haijatekeleza chochote tangu uhuru, jambo ambalo amesema ni kinyume na ukweli.

Wasira aliwataka wanachama wenye nia ya kugombea nafasi za uongozi kujitokeza bila kuogopa kuwa hawana fedha, akisema kiongozi anapaswa kuchaguliwa kwa uwezo, sifa na uadilifu, siyo kwa kutumia fedha kushawishi wapiga kura.

Akiwa Iramba, Wasira aliwakumbusha wana-CCM wenzake kuwa chama hakipaswi kuruhusu viongozi wanaopatikana kwa rushwa, vitisho au ujanja, akisisitiza kuwa viongozi wanapaswa kuchaguliwa kwa misingi ya haki na uwezo.

Kuhusu uimara wa viongozi, Wasira alisema viongozi hawapaswi kuyumba katika masuala ya msingi au kubadilisha misimamo kutokana na mazingira au maslahi binafsi.

Alisema utajiri siyo kipimo cha uwezo wa kuongoza. Kauli yake ilikuwa kwamba mtu hawezi kudai uwezo wake wa uongozi umeongezeka kwa sababu fedha zake zimeongezeka; kwa mtazamo wake, fedha haziwezi kuongeza uwezo wa mtu kuongoza.

Alisema uwezo wa kuongoza si jambo la kudumu maisha yote na kiongozi anapaswa kuwa tayari kumpisha mwingine pale anapoona uwezo wake hauendani tena na mahitaji ya wakati.

Aliwataka wanachama kutumia vikao rasmi badala ya kutegemea taarifa za mitandao ya kijamii.

Wasira alionya kuwa kuna taarifa nyingi zisizo za kweli kwenye mitandao na akashauri wanachama wakutane, wajadili madai yanayosambaa na watafute ufafanuzi kutoka kwa wenye ujuzi.

Katika ziara hiyo Wasira alitembelea Manyoni, Ikungi na Iramba, ikiwa na lengo la kuimarisha uhai wa chama na maandalizi ya uchaguzi wa ndani wa CCM unaotarajiwa mwaka 2027.

# Muafaka Z'Bar waendelea kukamilishwa

Na Mwandishi WETU, Pemba

MCHAKATO wa maridhiano ya kisiasa kati ya ACT Wazalendo na Chama Cha Mapinduzi (CCM) -Zanzibar, umeingia katika hatua mpya.

Hatua hizo ni kila upande wa vyama hivyo kukabidhi mapendekezo ya mfumo wa utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa baada ya mvutano wa kisiasa uliofuatia Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana - 2025, Pambazuko linaweza kudokeza.

Mwenyekiti wa ACT Wazalendo, Othman Masoud Othman, amewataka viongozi wa dini, masheikh, maimamu na Wazanzibari kwa ujumla kuunga mkono mchakato huo, akisema wakati umefika wa kuachana na tofauti za kisiasa na kuelekeza nguvu katika utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa.

Othman, ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar mstaafu, amesema pande hizo tayari zimepeana rasimu ya mapendekezo ya namna makubaliano hayo yatakavyotekelezwa. "Tumeshakabidhiana rasimu ya mapendekezo ya mchoro wa kuandaa utaratibu wa utekelezaji ili masuala haya yaweze kutekelezwa. Baada ya hapo itakuja tume itakayofanya kazi ya kutekeleza jambo moja baada ya jingine," alisema.

Alitoa kauli hiyo wiki iliyopita kisiwani Pemba wakati wa mkutano maalumu na viongozi wa dini ya Kiislamu, wakiwemo maimamu, masheikh na walimu wa vyuo vya Qur'an.

Makubaliano hayo yalifikiwa baada ya kutokuelewana kisiasa baada ya ACT Wazalendo kutoyakubali matokeo ya uchaguzi mkuu wa mwaka jana.

Hata hivyo, vyama hivyo vilikaa pamoja, kujadiliana na baadaye kutangazwa rasmi kwa maridhiano kupitia tamko la pamoja lililotolewa Ikulu ya Zanzibar Julai 9, mwaka huu.

Othman amesema kufikiwa kwa makubaliano hayo hakukuwa jambo rahisi, kutokana na tofauti kubwa za kisiasa zilizokuwepo na hitaji la pande mbalimbali kujenga uaminifu na maridhiano.




Othman amewataka viongozi hao kutumia nafasi na ushawishi wao katika jamii kuwaunganisha Wazanzibari na kujenga uelewa mpana kuhusu umuhimu wa mchakato wa maridhiano.

Amesema sasa ni wakati wa kuondoa mifarakano na kujenga umoja wa kweli wa Wazanzibari katika kutafuta suluhu ya kudumu ya changamoto za kisiasa.

### Maridhiano na uchumi

Kwa Othman, lengo la maridhiano siyo kumaliza tofauti za kisiasa pekee, bali pia kuweka mazingira yatakayoiwezesha Zanzibar kusonga mbele kiuchumi na kimaendeleo.

Amesema miongoni mwa vipaumbele vya makubaliano hayo ni kulinda maisha ya watu, mali zao na heshima yao.

Amesema mazingira ya amani na utulivu wa kisiasa ni muhimu katika kuwezesha Zanzibar kufikia maendeleo ya kiuchumi yanayostahili, akitoa mfano wa nchi nyingine zenye mazingira yanayofanana na Zanzibar ambazo zimepiga hatua kubwa kiuchumi.

Othman anatarajiwa kuendelea na ziara kama hiyo ya kukutana na viongozi wa dini na kwamba mikutano hiyo inatarajiwa kuwa sehemu muhimu ya juhudi za kujenga uelewa na kuhamasisha uungwaji mkono wa wananchi wakati Serikali ya Umoja wa Kitaifa ikielezea kwenye hatua ya kuanza kazi.

## Wazo Binafsi

# Siku ya Vijana Duniani na mustakabali wao Tanzania



Na Steven MBOGO

KILA ifikapo Agosti 12 kila mwaka, dunia husimama kwa muda kutafakari kuhusu vijana, siyo kwa sababu ni kundi linalohitaji huruma, bali wao ni moja ya nguvu kuu zinazoamua mwelekeo wa dunia ya sasa na ya kesho.

Mwaka 2026, siku ya vijana duniani iliadhimishwa chini ya kaulimbiu; "mazingira tofauti, matarajio yanayofanana." Hii inabeba ujumbe mzito.

Kwamba vijana wanaweza kuishi katika mazingira tofauti kabisa, lakini kwa ujumla wanatafuta mambo yanayofanana ambayo ni pamoja na heshima, fursa, usalama, elimu, ajira, uhuru wa kushiriki katika uamuzi na matumaini ya maisha bora.

Umoja wa Mataifa (UN) mwaka huu pia umeweka mkazo katika kuwapa vijana nafasi kubwa zaidi katika uamuzi wa ndani, kitaifa na kimataifa.

Kwa Tanzania, maadhimisho haya yanapaswa kuwa zaidi ya hafla ya kalenda. Yanapaswa kuwa kioo cha taifa; kioo kinachotuonyesha tulipo, tulichofanya kwa vijana wetu, tulichoshindwa kufanya, na muhimu zaidi, aina ya Tanzania tunayowaachia vijana wa leo kuirithi.

Kwa hiyo, swali la msingi katika siku hii ya vijana duniani siyo tumewafanyia nini vijana?" Swali pana zaidi ni; "Je, tumetengeneza Tanzania ambayo kijana anaweza kuishi, kufanya kazi, kubuni, kushiriki na kufanikiwa bila kulazimika kuondoka nchini ili kutafuta mustakabali wake?"

Hili ndilo swali ambalo Tanzania inapaswa kulijibu kwa uaminifu.

Tanzania ni taifa linalobadilika kwa kasi ya kidemografia. Vijana wa miaka kati ya 15 na 35 wanakadiriwa kuunda takribani asilimia 34.5 ya watu wote nchini, jambo linaloifanya Tanzania kuwa na moja ya nguvu kubwa za vijana katika muundo wake wa nguvu kazi.

Takwimu hii haipaswi kusomwa kama namba tu, bali kama taarifa ya kimkakati kuhusu mustakabali wa taifa.

Kwa sababu taifa lenye vijana wengi linaweza kupata kile kinachoitwa faida ya kiuchumi na kijamii inayoweza kutokea pale ambapo sehemu kubwa ya watu iko katika umri wa kufanya kazi, ikiwa taifa lina elimu bora, afya, ajira, ujuzi, uwekezaji na taasisi zinazowezesha uzalishaji.

Lakini mgawanyo wa kiuchumi, si zawadi inayokuja yenyewe, ni fursa inayohitaji maandalizi. Ikiwa vijana wana elimu lakini hawana ajira, mgawanyo wa kiuchumi inaweza kugeuka kuwa manufaa yatokanayo na hali ya kukatishwa tamaa.

Ikiwa wana nguvu lakini hawana fursa, nguvu hiyo inaweza kugeuka kuwa kukata tamaa. Ikiwa wana mawazo lakini hawana mazingira ya kuyatekeleza, ubunifu unaweza kuhamia nchi nyingine.

Inaendelea Uk. 23

# Siku ya Vijana...

Inatoka Uk. 22

Ikiwa wana haki ya kupiga kura lakini hawana nafasi ya kushiriki katika maamuzi, demokrasia inaweza kubaki kuwa tukio la siku moja badala ya kuwa utamaduni wa kila siku.

Kwa hiyo, Tanzania inapaswa kuelewa jambo moja la msingi: Idadi kubwa ya vijana siyo maendeleo. Ni uwezo wa maendeleo.

Maendeleo hutokea pale uwezo unapogeuzwa kuwa uzalishaji, uwekezaji na ujasiliamali.

Tatizo kubwa la mijadala yetu kuhusu vijana limekuwa ni tabia ya kuzungumza kuwahusu vijana badala ya kuzungumza pamoja na vijana.

Mara nyingi vijana huitwa kwenye mikutano, semina, kampeni na maadhimisho. Huitwa kusikiliza hotuba, kushangilia, kuhamasishwa na kuahidiwa. Lakini swali muhimu ni; Ni mara ngapi vijana wameketi mezani wakati uamuzi unaohusu maisha yao yanafanywa? Hapo ndipo tunapaswa kubadili fikra.

Vijana hawapaswi kuwa hadhira ya maendeleo, wanapaswa kuwa washirika wa maendeleo. Hawapaswi kuwa wapokeaji wa sera pekee, bali washiriki wa kutengeneza sera.

Hawapaswi kuwa nguvu ya kisiasa inayotafutwa wakati wa uchaguzi pekee. Wanapaswa kuwa sehemu ya mamlaka, uwajibikaji na uongozi wa taifa kila siku.

Kumwambia kijana 'wewe ni kiongozi wa kesho,' wakati unamnyima nafasi ya kuongoza leo ni kumwambia mtu mwenye uwezo wa kukimbia kwamba asubiri mpaka kesho ndipo apewe viatu.

Hakuna mjadala wa mustakabali wa vijana Tanzania unaoweza kuwa wa maana bila kuanzia kwenye ajira.

Takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) zinaonyesha kwamba, ukosefu wa ajira kwa vijana wenye umri wa miaka 15–35 ulikuwa 8.3, mwaka 2024, ukilinganisha na asilimia 9.7 mwaka 2020/21.

Hii ni hatua nzuri katika kipimo hicho, lakini haimaanishi kwamba tatizo la ajira kwa vijana limekwisha. NBS yenyewe inaonyesha kwamba vijana bado wana changamoto kubwa katika soko la ajira na kwamba tofauti za kijinsia zinaendelea kujitokeza.

Zaidi ya hapo, takwimu zinazohusiana na muda wa kufanyakazi zinaonyesha, upande mwingine wa simulizi.

Mtu anaweza kuhesabiwa kuwa ameajiriwa lakini akafanya kazi chini ya muda anaoweza na kutaka kufanya bila kipato kinachokidhi matarajio yake.

NBS inaeleza kuwa hicho ni kiashiria muhimu cha matumizi duni ya nguvu kazi, na pengo kati ya kazi iliyopo na uwezo au mahitaji ya mtu kufanya kazi zaidi. Hapa ndipo tunapopaswa kuwa waangalifu.

Ajira siyo kuwa na shughuli tu. Ajira ni kazi yenye tija, kipato kinachostahili, usalama na uwezo wa mtu kujenga maisha.

Kijana anayefanya biashara ndogo kwa siku nzima lakini hawezi kulipa kodi, kujenga nyumba, kuwekeza au kujiendeleza kielimu hawezi kusemwa kwamba tatizo lake limetatuliwa kwa sababu tu amejiajiri.

Moja ya mabadiliko makubwa ya Tanzania ni kuongezeka kwa kiwango cha elimu miongoni mwa vijana.

Utafiti wa Afrobarometer wa mwaka 2024 unaonyesha kwamba vijana wana elimu zaidi kuliko vizazi vilivyowatangulia, lakini wakati huo huo wanakabiliwa zaidi na changamoto ya ukosefu wa ajira.

Imebainishwa na utafiti huo kwamba takribani theluthi mbili ya vijana wangependa kuanzisha biashara zao wenyewe.

***Mwandishi wa makala haya ni mtafiti, mchambuzi na msomaji wa muda mrefu wa gazeti la Pambazuko.***



Kilinge cha Mawasiliano



Na Loth MAKUZA

# Mlanguzi wa binadamu hununua maneno sio silaha

VITA dhidi ya usafirishaji haramu wa binadamu haitashinda kwa sauti kubwa, bali itashinda kwa akili ya kimawasiliano.

Wapo vijana kutoka Pwani, Singida, Arusha, Mwanza, Tanga na Dodoma waliahidiwa mafunzo na kazi nzuri ya mauzo mkoani Morogoro.

Walipofika, waliwekwa katika mzunguko; walilazimishwa kununua bidhaa za bei mbaya, kisha wakafundishwa jinsi ya kuwashawishi wengine wafanye hivyo hivyo.

Wengi walifundishwa hata jinsi ya kuwadanganya familia zao kwamba wanapata pesa, hakuna aliyewafunga minyororo.

Hawa wote walishikwa kwa maneno, ahadi, mafunzo, mfumo wa "mafanikio" uliopangwa vizuri kiasi cha kuwafanya wawe sehemu ya udanganyifu wenyewe, hii siyo hadithi ya kubuni ni kesi halisi iliyoainishwa katika Ripoti ya Mwaka 2024/2025 ya Tanahut, ambao ni Mtandao wa Kitaifa wa Kupinga Usafirishaji Haramu wa Binadamu, iliyozinduliwa rasmi Agosti 20, 2026 jijini Dar es Salaam.

Ripoti hiyo mpya ya Tanahut, inaonyesha zaidi ya kesi 2,400 zilizoripotiwa Tanzania Bara katika kipindi kilichopita, nyingi zikitoka Ukanda wa Mashariki, hasa Morogoro, ambako pekee kunachangia takriban kesi 1,700.

Ukanda wa Ziwa Victoria; ikiwamo mikoa ya Kagera, Mwanza, Mara, Geita na Simiyu, unafuata kwa kesi 400, kutokana na ukaribu na Ukanda wa Maziwa Makuu, kazi za kilimo cha tumbaku na uchimbaji mdogo wa madini unaowavuta hata raia wa Uganda na Burundi.

Kwa aina ya unyonyaji, "uhalifu wa kulazimishwa" (forced criminality) ndio unaoongoza, zaidi ya matukio 1,000, ukifuatiwa na unyonyaji wa nguvu kazi na unyonyaji wa kingono.

Wavulana wanaonekana zaidi kwenye unyonyaji wa nguvu kazi; wasichana kwenye utumwa wa nyumbani na unyonyaji wa kingono. Hizi siyo namba tu, ni ramani ya jinsi walanguzi wanavyoongea na kila kundi kwa lugha yake.

Ni kujenga simulizi zinazopambana na ahadi za walanguzi bila kutengeneza hofu isiyo na tija, ni kufanya kazi na waandishi wa habari bila kumfichua muathirika mara ya pili kwa jina la habari kali.

Ni kuunganisha serikali, mashirika kama Tanahut ambao ni muungano wa taasisi 105 nchini, vyombo vya habari na sekta binafsi chini ya sauti moja.

Na hapa ndipo tunapaswa kujiuliza swali ngumu; je, tunawasiliana ili kulinda watu au tunawasiliana ili kuonyesha shirika letu linafanya kitu?

Kampeni yenye "views" milioni moja inaweza kuwa sahihi kiuandishi lakini mbaya kimaadili, hasa pale muathirika anapogeuzwa kuwa kielelezo cha kutengeneza huruma badala ya binadamu mwenye heshima na faragha yake.

Sekta binafsi nayo haiwezi kujitoa, kampuni za ajira, uchimbaji madini, kilimo na usafirishaji ndio yanayokutana na waathirika kabla ya mtu mwingine yeyote.

Sera nzuri ya ajira ya haki, ikiwasilishwa vizuri, ni kinga.

Walanguzi wa binadamu hawapigani kwa nguvu tu, bali kwa maneno yaliyopangwa vizuri na kumlenga mtu sahihi na wakati sahihi.

Hadi tutakapoelewa hilo, tutaendelea kuchapisha mabango wakati wao wanajenga mifumo mizima ya "mafunzo" inayogeuza waathirika kuwa mawakala wapya wa udanganyifu.

Vita hii haitashinda kwa sauti kubwa zaidi, itashinda kwa mawasiliano ya karibu zaidi, ya mapema zaidi na yenye akili zaidi kuliko ya adui.

Mwandishi wa safu hii ni mtaalamu wa Uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: na kupitia email; projects@ lothmakuza.co.tz.

Chanzo: Ripoti ya Mwaka 2024/2025 ya Tanahut, iliyozinduliwa Agosti 20, 2026, Dar es Salaam.

***Mwandishi wa safu hii ni mtaalamu wa Uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@ lothmakuza.co.tz***

Na Emmanuel JACOB



# Kwa nini watumiaji wa 'wheelchair' husukumwa?



MARA nyingi ukitembea mtaani, hasa mijini, utaona mtu aliyeketi kwenye kiti-mwendo (wheelchair), anasukumwa na mtu mwingine.

Inaonekana kama kitendo cha kutoa msaada au wema wa kawaida, lakini ukichunguza kwa undani, taswira hii inafichua ukweli mchungu kuwa tumeruhusu dhana potofu na miundombinu mibovu kumpokonya mtumiaji wa kiti-mwendo uhuru wake.

Kimsingi, kiti-mwendo hakikubuniwa ili kumfanya mtu awe tegemezi wa kusukumwa kila mahali; ilibuniwa kuwa chombo cha kumfanya mtu ajitegemee na atembee kwa uhuru wake mwenyewe. Lakini kwa nini kila tunayemwona mjini leo anasukumwa?

Kwa wasomaji wa gazeti la Pambazuko makala hii imeangazia baadhi ya sababu zinazopelekea jambo hili angalau kwa ufupi ambazo ni pamoja na mchanganyiko wa mazingira magumu, sababu za kiafya, au wakati mwingine, ukosefu wa uelewa wa kijamii.

Mazingira yasiyofikika: Mitaa yetu imejaa ngazi ndefu, barabara zisizo na sehemu rasmi ya kushika (ramps), miundombinu mibovu na kando za barabara zilizoinuka mno. Katika mazingira kama haya, kujisukuma mwenyewe inakuwa vigumu.

Uchovu wa kimwili; kujisukuma mwenyewe kunahitaji nguvu kubwa ya mikono na kifua.

Mtu anaposafiri umbali mrefu katikati ya mji, akiwa anatumia manual wheelchair, uchovu unamlazimu kutafuta msaada.

Hali za kiafya na majeraha; Watu wenye hali kama vile kupooza mikono, kiwiliwili na miguu, ugonjwa wa mfumo wa fahamu (Multiple Sclerosis), au wale wanaouguza majeraha ya muda mfupi, wanaweza kukosa uwezo wa kutosha wa mikono au nguvu za kujisukuma.

Pamoja na kwamba kutoa msaada ni jambo la kiutu, kuna tatizo kubwa linalojitokeza mara kwa mara: watu kuwasukuma watumiaji wa viti mwendo na wakati mwingine bila hata kuwaomba ridhaa au idhini.

Kitendo hiki kinachukuliwa na wengi kama wema, lakini katika ulimwengu wa kisasa na haki za watu wenye ulemavu, ni ukiukaji mkubwa wa mipaka ya mtu.

Kiukweli ni muhimu jamii ifahamu kumsukuma mtumiaji wa kiti mwendo hupoteza uhuru wake kujiamulia.

Unamnyima mtu haki ya kuchagua wapi aende, kwa kasi gani, na kwa wakati gani. Vilevile, humfanya mtu aonekane kama mtoto.

Kitendo hiki kinajenga taswira kwamba mtu mwenye ulemavu ni dhaifu, hawezi kujifanyia maamuzi, na anahitaji "kusaidiwa" kila wakati.

Ni wakati sasa wa kubadili mtazamo wetu kama jamii. Usawa wa kweli sio tu kutoa msaada; ni kutengeneza mazingira yanayomwezesha kila mtu kujitegemea na kuheshimu utu na mipaka ya kila binaadamu.

***Mwandishi: Emmanuel Jacob, Ofisa Mfiziotherapia (Mwenyekiti wa Tanzania Physiotherapy Initiative). Simu: 0765359305 Instagram: Emmanuel Jacob***



Bustani ya Sheria

Na Wakili Karim Gabriel Mussa

# Sakata la Wakili Fatma Karume – V



KATIKA sehemu ya nne tuliona jinsi Mahakama Kuu ilivyotengua uamuzi wa Kamati ya Maadili ya Mawakili uliokuwa umemfuta Wakili Fatma Karume kwenye Daftari la Mawakili.

Sababu haikuwa kwamba Mahakama ilisema Fatma hakufanya kosa. La hasha, bali ilisema utaratibu uliotumika kuifikisha kesi mbele ya Kamati haukufuata agizo la awali la Mahakama, kwani aliyepaswa kuipeleka ilikuwa ni Msajili wa Mahakama Kuu, siyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kwa wengi, huo ulikuwa ushindi mkubwa kwa Fatma Karume, lakini serikali haikuwa tayari kukubali kushindwa.

Baada ya Mahakama Kuu kutengua uamuzi wa Kamati ya Maadili, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Kamati ya Maadili walitaka kupeleka shauri hilo Mahakama ya Rufani, lakini kulikuwa na kikwazo kimoja muhimu.

Kwa mujibu wa sheria, hawangeweza kukata rufaa moja kwa moja kwani walipaswa kwanza kupata ruhusa (leave) kutoka Mahakama Kuu.

Hivyo wakafungua maombi wakiiomba Mahakama Kuu iwape ruhusa ya kukata rufaa.

Upande wa Fatma Karume, ukiwakilishwa na Wakili Peter Kibatala pamoja na Dkt. Rugemeleza Nshala, uliipinga hoja ya serikali.

Kwa kifupi, waliieleza Mahakama kwamba haikuwa imeonyesha hoja mpya nzito zinazostahili kujadiliwa Mahakama ya Rufani.

Uamuzi wa Mahakama Kuu ulikuwa umejengwa kwenye misingi sahihi ya sheria. Hakukuwa na sababu ya kuiruhusu Serikali kuendelea na rufaa nyingine.

Kwa hiyo, waliomba maombi hayo yatupiliwe mbali.

Mahakama ya Tanzania (Kuu) ikaamua baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, Mahakama Kuu ilifikia uamuzi wake na kutamka kuwa serikali haikuonyesha hoja za msingi (arguable points of law) zinazohitaji kuamuliwa na Mahakama ya Rufani.

Kwa sababu hiyo, Mahakama ikakataa kutoa ruhusa (leave) ya kukata rufaa na kwa lugha rahisi serikali ilishindwa hatua ya kwanza kabisa.

Haikuruhusiwa kwenda Mahakama ya Rufani kupitia njia hiyo, je, hapo ndipo kesi iliisha? Wengi walidhani ndiyo, lakini serikali haikukata tamaa.

Badala ya kuishia hapo, serikali Iliamua kujaribu tena na safari hii haikurudi Mahakama Kuu.

Iligonga moja kwa moja mlango wa Mahakama ya Rufani, ikiomba ruhusa hiyo hiyo ambayo ilikuwa imekataliwa na Mahakama Kuu.

Katika taaluma ya sheria, hatua hiyo mara nyingi huitwa "second bite" yaani kujaribu tena kupata ruhusa baada ya kunyimwa katika mahakama ya chini.

Lakini hata safari hiyo haikuwa rahisi, kwani kulikuwa na pingamizi jingine la kiufundi lililowakabili kabla hata Mahakama ya Rufani haijafikiria kama wapewe ruhusa au la.

Je, pingamizi hilo lilikuwa nini? Na Mahakama ya Rufani ililiamuaje?

Hapo ndipo simulizi hili linaingia katika hatua ya sita.

Itaendelea...

***Mwandishi ni Mwanasheria na Mchambuzi wa Sheria kutoka KGM Attorneys). Anapatikana kwa namba: 0755 395 572 au Email: karimbinmussa@gmail.com***



Na Rashid MTAGALUKA

Hoja Yangu

# Faida za JNHPP zipige hodi majumbani

KUKAMILIKA kwa Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), unaofahamika pia kama Stiegler's Gorge, ni hatua kubwa katika historia ya nishati Tanzania.

Mradi huo wenye uwezo wa kuzalisha megawati 2,115 umejengwa kwa gharama ya takribani Shilingi trilioni 7.45, ukiwa miongoni mwa uwekezaji mkubwa zaidi wa miundombinu nchini.

Lakini baada ya miaka ya ujenzi na matumizi makubwa ya fedha za umma, swali la msingi sasa siyo tena kama mradi umejengwa. Swali ni utaleta faida gani katika maisha ya Mtanzania?

Kwa uwezo wa megawati 2,115 na makadirio ya kuzalisha takribani gigawati-saa 5,920 kwa mwaka, JNHPP ina uwezo wa kubadilisha sura ya sekta ya umeme na uchumi kwa ujumla.

Mradi ulianza kuingiza umeme kwenye gridi kwa awamu mwaka 2024, ukiwemo mchango wa awali wa megawati 235.

Hii ni nafasi ambayo Tanzania haipaswi kuiacha ipite. Umeme mwingi na wa uhakika unatakiwa kuwa kichocheo cha viwanda, kilimo cha umwagiliaji, biashara, huduma za kidijitali na ajira.

Hoja Yangu hapa ni serikali inapaswa kuhakikisha kwamba umeme huu hauishii kwenye takwimu za mafanikio, bali unaonekana kwenye uzalishaji wa bidhaa na huduma.

Takwimu za Benki ya Dunia zinaonyesha kuwa mwaka 2023 ni asilimia 48.3 tu ya Watanzania waliokuwa na upatikanaji wa umeme.

Hii ina maana kuwa, licha ya uwekezaji mkubwa katika uzalishaji, bado kuna kazi kubwa ya kupeleka umeme kwa wananchi.

Kwa maana hiyo, hatua inayofuata inapaswa kuwa kuongeza kasi ya usambazaji.

Umeme wa JNHPP ukifika vijijini, unaweza kubadilisha maisha kwa kuwezesha mashine za kusaga na kukoboa, viwanda vidogo, vituo vya kuhifadhi mazao, visima vya maji saloon za vijana na huduma za afya na elimu.

Benki ya Dunia tayari imeonesha mifano ya maeneo ambako upatikanaji wa umeme umewezesha biashara ndogo na viwanda kukua,



huku uzalishaji wa mpunga na mafuta ya alizeti ukiongezeka na gharama za usafirishaji kupungua.

Ndiyo maana Serikali inapaswa kuwa na mpango mahsusi wa kuhakikisha umeme huu unazalisha thamani ya kiuchumi.

Viwanda vipya vinapaswa kuvutiwa, vilivyopo viwezeshwe kupanua uzalishaji, na wawekezaji wa ndani wahamasishwe kutumia fursa ya nishati ya uhakika.

Vilevile, wananchi wanahitaji kuona uwazi kuhusu gharama za mradi, mapato yanayotarajiwa na namna uwekezaji huo utakavyorejesha thamani kwa Taifa.

Kwa hiyo, mafanikio ya Stiegler's Gorge hayatapimwa kwa ukubwa wa bwawa wala idadi ya megawati pekee.

Yatapimwa kwa viwanda vingapi vitaongezeka, ajira ngapi zitazalishwa, uzalishaji utakua kwa kiasi gani na maisha ya wananchi yatabadilika kwa kiwango gani.

Sasa ni wakati wa kugeuza megawati kuwa maendeleo. Hapo ndipo Stiegler's Gorge itakapothibitisha kuwa siyo tu mradi mkubwa wa umeme, bali ni uwekezaji mkubwa katika maisha ya Mtanzania.

***Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com***

Makala

# Pengo elimu afya ya uzazi tishio ustawi wa vijana - I



Na Elizabeth MWINUKA, Dodoma

MKOA wa Dodoma una zaidi ya theluthi moja ya wakazi wake wakiwa vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 35.

Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, inaeleza kuwa wakazi wa mkoa huo wanafikia 765,179, huku vijana wakiwa asilimia 33.5.

Hata hivyo, kundi hilo ambalo linatarajiwa kuwa nguvu kazi ya taifa, ndilo linalokabiliwa na pengo kubwa la elimu ya afya ya uzazi, hali inayochochea mimba za utotoni, maambukizi ya magonjwa ya zinaa na kusitishwa kwa masomo kwa maelfu ya wasichana.

Takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 29 ya wasichana mkoani Dodoma wamewahi kupata ujauzito. Hii inaamanisha kuwa msichama mmoja katika kila wasichana watatu mkoani humu, amepata ujauzito.

Takwimu hizo zinaonyesha kuwa tatizo siyo la mtu mmoja mmoja, bali ni changamoto ya afya ya umma.

Utafiti wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), unaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 60 ya wasichana wenye umri wa miaka 15 hadi 19 wana uelewa mdogo kuhusu afya ya uzazi, huku asilimia 22.3 pekee wakitumia njia za kisasa za uzazi wa mpango.

Watafiti walihitimisha kuwa ukosefu wa elimu sahihi ya afya ya uzazi ni moja ya sababu kuu zinazochochea ujauzito wa utotoni katika mkoa huo.

**Sheria zipo, uwajibikaji haupo**

Tanzania ina Sheria ya Afya ya Umma ya mwaka 2009, Sheria ya Kudhibiti VVU na UKIMWI ya mwaka 2008 pamoja na Sheria ya Ubora Huduma za Afya kwa Vijana - mwaka 2020 ambapo zote zinataka vijana wapate huduma rafiki na elimu sahihi ya afya ya uzazi.

Lakini uchambuzi wa utafiti mbalimbali unaonyesha pengo kubwa la utekelezaji. Ni asilimia 65 pekee ya vituo vya afya nchini vinavyokuwa na nakala za sheria hizo huku asilimia 31 ya vituo vya usimamizi wa huduma za afya ya uzazi vikishindwa kufanya majukumu yake kwa kufuata taratibu za kutoa elimu na huduma kwa mwaka.  Hiki ni kiwango cha juu sana ukilinganisha na wastani wa kitaifa wa asilimia 27.7, jambo ambalo linaibua mahitaji ya hatua za kuchukuliwa ili kulishughulikia tatizo hilo.

Watu ambao wamehojiwa na gazeti hili kuhusiana na suala hili wanasema halitokani na umasikini au uhusiano wa utotoni pekee, bali pia linatokana na pengo kubwa la elimu sahihi ya afya ya uzazi linalowaacha maelfu ya vijana wakifanya uamuzi muhimu wa maisha bila taarifa za kutosha.

Inaendelea Uk. 29

# Stadi za maisha...

Inatoka Uk. 28

Tatizo hilo linaonekana pia katika kiwango cha uelewa wa vijana. Mathalan, utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kwa wasichana 539, ulibaini kuwa zaidi ya asilimia 60 walikuwa na uelewa mdogo kuhusu afya ya uzazi, huku ni asilimia 22.3 pekee wakitumia njia yoyote ya kisasa ya uzazi wa mpango.

Watafiti walihitimisha kuwa vijana wenye uelewa mdogo walikuwa katika hatari kubwa zaidi ya kupata ujauzito wa utotoni. Na utafiti uliofanywa na gazeti hili umethibitisha hilo.

Licha ya Tanzania kuwa na sera, sheria na miongozo inayotambua haki ya vijana kupata elimu na huduma za afya ya uzazi, uchunguzi huu unaonyesha kuwa katika maeneo mengi ya Jiji la Dodoma, ikiwemo UDOM, Makulu, Ntyuka, Ng'ong'ona na Iyumbu, elimu hiyo bado hutolewa kwa vipindi maalumu kupitia kampeni na semina badala ya kuwa sehemu ya mfumo endelevu unaowafikia vijana wote.

**Ushahidi**

Matokeo ya utafiti huo yanaonyesha kuwa changamoto ya afya ya uzazi kwa vijana siyo suala la tabia binafsi pekee, bali pia ni matokeo ya ukosefu wa taarifa sahihi.

Utafiti ulibaini kuwa takribani asilimia 94 ya washiriki wa utafiti walikuwa tayari wameanza kushiriki ngono, huku robo yao wakianza kabla ya kufikisha umri wa miaka 14.

Kutokana na kutokuwa na elimu sahihi ya afya ya uzazi, hata matumizi ya huduma za uzazi wa mpango yalikuwa ya chini sana miongoni mwa vijana waliofanyiwa utafiti.

Hali hiyo inaendana na ushahidi mwingine unaoonyesha kuwa bado mfumo wa huduma haujawa rafiki kwa vijana.

Tafiti zinaonyesha kuwa asilimia 84 ya watoa huduma za afya bado huwashauri vijana kuacha kabisa kushiriki ngono wanapofika kutafuta ushauri kuhusu uzazi wa mpango badala ya kuwapatia taarifa kamili zinazowawezesha kufanya maamuzi salama.

Aidha, ni asilimia 23 pekee ya vituo vya afya nchini vina wafanyakazi wenye umri chini ya miaka 25, jambo linalopunguza ukaribu kati ya vijana na watoa huduma.

Jambo hilo linaongeza uwezekano wa mimba zisizotarajiwa na maambukizi ya magonjwa ya zinaa. Si ajabu takribani asilimia 30 ya wasichana wa Dodoma wamejikuta wakipata ujauzito.

Katika eneo la Ng'ong'ona, kijana mmoja mwenye umri wa miaka 21 anasema hakuwahi kupata darasa la afya ya uzazi tangu amalize sekondari.

"Elimu huwa inatolewa wakati wa kampeni au maadhimisho. Baada ya hapo hakuna anayekuja tena. Wengi wetu tunajifunza kupitia marafiki au mitandao ya kijamii," anasema.

Kauli hiyo ilijirudia kwa vijana wengine waliokutwa Makulu, Iyumbu na Ntyuka, ambapo wengi walieleza kuwa semina za afya ya uzazi hutegemea uwepo wa mashirika yasiyo ya kiserikali au miradi ya muda mfupi.

* Itaendelea toleo lijalo...

**** Mwandishi ni mwanafunzi wa shahada ya uandishi wa habari katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).***



# Barua za Wasomaji



**Tunakaribisha barua. Tuma kupitia**

**Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz**

## Watoto wa mitaani wasipuuzwe

**Mhariri,**

UWEPO wa watoto wa mitaani limekuwa tatizo sugu katika miji mikubwa hapa nchini.

Uwepo wao mitaani unazalisha watoto wasiosoma.

Mtoto aliyekuwa mtaani bila shule, akikomaa anaunda familia bila elimu, watoto wake nao wanaingia mtaani. Hivi ndivyo umaskini na ujinga unavyozaliana kizazi baada ya kizazi.

Hawa siyo wahuni, ni wahanga wa nyumba zilizovunjika, umaskini na shule zilizowafukuza. Leo wanakula mabaki, kesho watakuwa wazazi wa watoto wengine wa mitaani.

Serikali na jamii lazima tuingilie, tujenge vituo vya ufundi, tuwarudishe shule na tuwapatie malezi.

Kama hatutafanya sasa, baada ya miaka kumi tutakuwa na jiji la watu wasiojua kusoma. Kamwe jamii zisinyamaze tuwaokoe leo.

**Neema Juma**
**Sanawari, Arusha.**

## Magari ya vyombo vya usalama viko juu ya sheria?

**Mhariri,**

INASIKITISHA kuona baadhi ya magari ya Jeshi la Polisi, Jeshi la Wananchi na Magereza yamekuwa yakivunja sheria za usalama barabarani wazi wazi.

Inashangaza sana kwa sababu vyombo hivyo vya usalama ndiyo vinapaswa kuwa mfano wa usimamizi wa sheria.

Mfano mara kadhaa tumekuwa tukishuhudia magari ya vyombo hivyo vya usalama, yakipita kwenye barabara isiyo sahihi na hata kukiwa na taa nyekundu yamekuwa yakipita spidi kubwa na kumdharau hata askari anayeongoza magari.

Tunajiuliza wakati wote wao ndiyo wana haraka kuliko wananchi au wako juu ya sheria? Kibaya zaidi wakati mwingine magari haya yamekuwa yakisababisha ajali na hata pale wanapogonga gari yako wanaondoka bila kujali.

Tunaomba mamlaka husika ichukue hatua katika hili maana ni aibu kuona vyombo vya ulinzi na usalama, vinakuwa mstari wa mbele kuvunja sheria.

**Raphael Edison,**
**Mwenge, Dar es Salaam**

## Serikali iweke wazi mustakabali wa IPTL

**Mhariri,**

SISI tuliokuwa wafanyakazi wa kampuni ya kufua umeme ya Independent Power Tanzania Limited (IPTL), tunaiomba serikali kuingilia kati na kuweka wazi hatma ya mgogoro wa malipo kati yetu na kampuni hiyo.

Hivi sasa tunanyanyaswa na mmoja wa viongozi waliokuwa wakubwa wetu ambapo anataka kutuondoa kwa nguvu kwenye nyumba tulizopewa kama makazi wakati tunasubiri kulipwa mafao yetu.

Sisi tulipewa nyumba hizo na uongozi wa kampuni hiyo kwa ajili ya kulinda mitambo, magari pamoja na nyumba kadhaa zilizokuwa makazi ya maofisa wa kiwanda.

Tumeshangaa sasa tumepewa notisi za kuondoka bila kupewa maelezo ya kina kwa nini tunaondolewa.

Lakini tunazo taarifa kwamba kuna mchezo mchafu unafanywa ili kuuza nyumba hizo bila serikali kujua.

Tunaamini kupitia gazeti hili, serikali itaingilia kati na kuzima hujuma zozote zinazopangwa kulihujumu taifa letu.

**Mimi mfanyakazi wa IPTL,**
**Dar es Salaam.**


MOVE FOR DISABILITY
INCLUSION BY DESIGN 26'
CHANGIA LEO!
Mchango wako utasaidia kupatikani kwa vifaa muhimu kwa watu wenye changamoto ya mjongeo kama vile miguu bandia, viti mwendo, fimbo za kutembelea n.k.
TIPS
selcom
MOVE FOR DISABILITY
6124 6810
Maliza
MOVE FOR DISABILITY
6 1 2 4 6 8 1 0
INCLUSION BY DESIGN 26'
SPONSERED BY
UHURU
circleg
Pambazuko

# Habari katika Picha




*Rais Samia Suluhu Hassan akizindua rasmi Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Julius Nyerere (JNHPP) chenye uwezo wa kuzalisha megawati 2,115, juzi Agosti 22 2026, katika eneo la mradi lililopo Rufiji, mkoani Pwani. (Picha na Ikulu)*




*Meneja wa Mfuko wa PSSSF Kanda ya Kinondoni, Costa Mpagike (aliyesimama), akitoa hotuba ya ufunguzi wa mafunzo ya siku mbili kwa waandishi wa habari kuhusu Hifadhi ya Jamii. Ikiwa ni sehemu ya jitihada za kuongeza uelewa wa umma na wanachama kuhusu huduma, haki na wajibu unaotolewa na mfuko huo. Ufunguzi huo ulifanyika Agosti 17, 2026. Wengine pichani ni Ofisa Uhusiano Mkuu PSSSF, Abdul Njaidi (kushoto) na Mratibu wa mafunzo hayo, Nevile Meena.*



*Naserian na Naipoi Onesmo Olengurumwa, wakikumbatiwa na wazazi wao wakati wa mahafali ya kuhitimu darasa la saba katika Shule ya Msingi Bright Hope Schools, juzi jijini Dar es Salaam. Picha na Mpigapicha WETU.*


Bati/ Mtu, Mtu Bati
HATUCHOKI!
Changia kupitia
NMB A/C NO 31910046325
ELCT KARAGWE IRON SHEET PROJECT
CRDB A/C NO 0150764151900
UWAKILI PROJECT ELCT KAD
Mawasiliano:
0754 742 423
Askofu Benson K Bagonza

Na Anti MSHAURI





# Fanya yote, usimsahau Mungu

NI wiki nyingine tena tunakutana katika safu hii ya uhusiano ili kufahamishana mambo mbalimbali ya maisha.

Wiki iliyopita nilizungumza umuhimu wa wazazi kutenga muda wa kukaa na watoto wao na wiki hii nitazungumza namna ya kufanya mambo yako bila kumsahau Mungu kwa kumpatia shukrani na maombi.

Katika maisha ya kila siku tunakimbia shule, kazi, biashara na familia lakini wengi wetu tumekuwa tukimsahau Mungu na kuegemea kwenye maisha ya kidunia pekee bila kufahamu kuwa mafanikio yetu bila msingi wa kiroho ni kama nyumba iliyojengwa juu ya mchanga.

Ikiwa utatumikia Mungu na mali utakuwa umetimiza wajibu wa msingi katika maisha yaani kuonyesha bidii, nidhamu na uwajibikaji.

Mungu ametupa akili, nguvu na muda. Kuyatumikia vizuri majukumu yetu bila kumsahau na katika huduma kwa wengine ni ibada pia.

Kutomsahau Mungu ni kumbusho la kushukuru na kuomba mwongozo kutoka Kwake.

Tunapopanga bajeti, kuchagua marafiki, au kufanya maamuzi makubwa na kumweka Mungu mbele hutupa hekima na amani. Sala, toba na matendo mema vinatufundisha unyenyekevu na huruma.

Kwa jamii zetu tunazoishi kwa ujumla, ujumbe huu unatufundisha usawa; shughulika na dunia lakini shika na mbingu. Wazazi wafundishe watoto bidii na maadili, viongozi watumikie kwa uadilifu. Vijana wafanye kazi na pia waweke muda wa ibada na kujifunza.

Tufanye yote kwa mikono yetu na mioyo yetu ikiwa kwa Mungu, tunajenga jamii yenye maendeleo, upendo na matumaini ya kweli.

Tukutane wiki ijayo

***Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.***

# Pekosi; mtindo wa zamani uliorudi kwa kasi



VAZI la pekosi ni aina ya suruali inayoshika mwili kuanzia usawa wa kiuno hadi kwenye magoti, lakini kushuka chini huachia tofauti na suruali za kawaida.

Mtindo huo wa suruali ulivaliwa sana miaka ya zamani kabla ya kuingia staili ya "skin jeans" ambayo muundo wake hushika mwili kuanzia sehemu ya kiunoni hadi chini miguuni.

Baada ya "skin jeans" kuvaliwa kwa miaka mingi, sasa mtindo wa pekosi kwa wanawake umerudi kwa kasi.

Vazi hili linawapendeza wengi kwa sababu linaonyesha umbo la mwili vizuri na linafaa kwa miili tofauti ambapo linaficha tumbo kidogo na ku-balance hips.

Pekosi linafaa kuvaa ofisini, kwenye sherehe au hata katika mtoko wa kawaida.

# Tunza "lips" zako hivi

KUTUNZA midomo (lips) ni muhimu sana kwa afya na muonekano wako, kwa sababu midomo haina tezi za mafuta kama sehemu nyingine za ngozi hivyo hukauka haraka.

Ukikosa kuitunza midomo, inaweza kupasuka na kusababisha maumivu.

Midomo iliyopasuka inaweza kuruhusu bakteria na vijidudu kuingia mwilini na kusababisha maambukizi.

Dondoo za kutunza midomo

* Kunywa maji ya kutosha
* Tumia lip balm mara kwa mara
* Epuka kulamba midomo mara kwa mara
*Kula vyakula vyenye vitamin E na C
*Linda midomo dhidi ya jua na baridi







# Dogo Janja: Madee alitaka nisome siyo muziki

Na Mwandishi WETU

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Abdulaaziz Chande maarufu Dogo Janja, amesema msanii mwenzake, Madee alitaka asome na si kufanya muziki.

Dogo Janja ambaye pia ni Diwani wa Ngarenaro jijini Arusha, ametoa kauli hiyo wakati akihojiwa kwenye shoo ya miaka 30 ya Bongo Fleva iliyofanyika Dodoma juzi Agosti 22,2026.

"Unajua wakati Madee ananichukua na kunileta Dar es Salaam nilikuwa mtoto mdogo kabisa, alitaka nisome kwanza na sio kufanya muziki lakini ndiyo hivyo tena,"amesema Dogo Janja.


# Jux aachia video ya wimbo wake mpya

Na Mwandishi WETU

MSANII wa Bongo Fleva, Juma Jux ambaye kwa sasa anaishi nchini Nigeria tangu afunge ndoa, ameachia video ya wimbo wake (Sexy & Bad) aliyomshirikisha Staa wa muziki kutoka Ghana, StoneBwoy.








*Beki wa kati wa Timu ya Hull City, Nobel Mendy akishangilia bao lake la pili alilofunga katika mchezo wao dhidi ya Manchester United juzi. (Picha na George Wood)*

# Arsenal moto uleule, United Hoi!

**Na John MARWA**

MABINGWA watetezi Ligi Kuu ya England (EPL), Arsenal 'The Gunnners' wameuwasha moto na kusimamisha bendera kwa msimu mpya wa 2026/27 baada ya kuwakaribisha Coventry kwa kichapo cha mabao 3-0.

Mtanange huo ulirindima Ijumaa, Agosti 21 katika Dimba la Emirates jijini London, ukiwa ni mchezo wa kwanza wa msimu, ambapo ulitazamwa na mashabiki 60,098 kati ya 60,704 wanaopaswa kuujaza uwanja huo.

Mabao ya Arsenal yaliwekwa kambani na Kai Havertz, Bukayo Saka na Martin Odegaard. Ni mchezo ambao washika mitutu hao waliutawala kwa kiwango kikubwa, wakiwa na umiliki wa kandanda wa asilimia 64, wakipiga mashuti 20 huku sita yakilenga lango, na usahihi wa pasi ukiwa asilimia 92.

Wakati Arsenal wakipepewa kwa ushindi, mahasimu wao Manchester United wameuanza msimu kwa kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Hull City, mchezo ulipigwa kwenye dimba la MKM, mjini Hull.

United walionyesha kiwango kibovu kwenye mchezo huo huku timu ikionyesha kukosa muunganiko katika maeneo matatu ya uwanja, eneo la ulinzi, kiungo na ushambuliaji, timu ilionekana kuwa wazi maeneo nyeti na kuwafanya wapinzani wao kutamba.

Ni kama mashabiki wa 'Mashetani Wekundu' walianza kujisahau kuwa bado timu yao haijakaa sawa, lakini mchezo mmoja umeanza kutonesha kidonda cha kukosa timu ya upinzani na zaidi ya miaka 14 hawajatwaa taji la EPL, licha ya kuwa mabingwa wa kihitoria sambamba na Liverpool ambapo timu zote zimetwaa mara 20.

Swali ni hili; je, ni kwa namna gani kocha wao, Michael Carrick atayatumia maingizo mapya ndani ya timu kufukia mashimo ambayo yameonekana mapema kuigharimu timu?



# Simba wayamalize na FVS



Na John MARWA

KUNA haja ya Klabu ya Simba na teknolojia ya 'Football Video Support' (FVS) kuyamaliza mapema kabla mambo hayajawa makubwa katika michezo ya Ligi Kuu ya NBC PL, 2026/27.

Ikiwa ni baada ya mizunguko mitatu ya mwanzo, wachezaji watatu wa Simba kuonyeshwa kadi nyekundu mtawalia.

Katika mchezo wa kwanza, Simba walipata kadi nyekundu kwa mlinzi wao wa kulia David Kameta kuonyeshwa kadi nyekundu baada ya FVS kumsaidia mwamuzi, katika tukio ambalo alimcheza vibaya mchezaji wa Kagera Sugar.

Adhabu hii ilikuwa ni wakati wa mchezo wa timu hiyo ya Msimbazi, Dar es Salaam na Kagera ambapo Simba waliibuka na ushindi wa mabao 2-0. Mabao hayo yaliwekwa kimiani na Ismael Toure na Ellie Mpanzu.

Katika mchezo wa pili uliopigwa katika Dimba la Kirumba, Mwanza dhidi ya Pamba Jiji FC, kiungo wa Simba, Ibrahim Jabaar alionyeshwa kadi nyekundu baada ya FVS kumkuta na hatia ya kumpiga kiwiko nyota wa Pamba.

Mtanange huo ulitamatika kwa Simba kuibuka na ushindi wa mabao 2-1. Mabao yalipachikwa na Clatous Chama na Anicet Oura.

Katika mchezo wa tatu, Simba pia akaangukia kwenye Mahakama ya FVS ambapo ilimkuta na hatia kwa Anthony Mligo kukutwa na hatia baada ya kucheza vibaya.

Hata hivyo wekundu wa msimbazi walifanikiwa kuondoka na alama tatu katika mchezo huo kwa kupata ushindi wa mabao 2-1, mabao yaliyofungwa na Clatous Chama na Rushine De Reuck aliyefunga kwa mkwaju wa penati.

Katika michezo mitatu Simba wamepata pigo la nyota wao kuonyeshwa kadi nyekundu na kulazimika kucheza pungufu, jambo ambalo limeonyesha kuiweka timu katika mazingira magumu hasa baada ya kuwapoteza nyota muhimu kwenye mechi ngumu.

Sasa basi, ni hatari zaidi kwa Simba kupewa adhabu kubwa kwa wachezaji wake kucheza vibaya kinyume na taratibu na kanuni za mpira wa miguu, hivyo ni wakati muafaka kwa timu hiyo kubwa kujitafakari na kuchukua hatua haraka ili kukwepa adhabu na hasara zinazoweza kuigharimu Simba.

*GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION